**28 AGOSTI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

### Kikao cha Pili – Tarehe 28 Agosti, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu tumekuwa tukisemasema jambo hili na sasa limetimia. Nitumie fursa hii kwa niaba yenu ninyi nyote na Watanzania wote kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *WHO* (Shirika la Afya Duniani) Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Uchaguzi huo umefanyika jana na kazi nzuri sana imefanyika kwa maana ya kampeni zilizopigwa kuanzia kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hatua mbalimbali ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alizichukua kwanza yeye mwenyewe kuzungumza na Wakuu wa Nchi wenzake wa Afrika, pia kufika mahali ambapo yeye mwenyewe akaona ngoja azungumze ili wamsikie Watanzania wote na Waafrika wote, sote tumeona. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa kweli kwa hatua hizo ambazo amezichukua kwenye ngazi hiyo ambayo imemsaidia Mbunge mwenzetu kupata hiyo nafasi. Kwa hiyo na Mheshimiwa Rais naye tunampongeza kwa sababu sote tunafahamu ni wanasiasa, ukiingiza miguu yote miwili kwenye jambo unatamani ufanikiwe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili kubwa lililotokea, ni heshima kubwa kwa nchi yetu kwa kweli ametuletea na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile tutampa salamu hizo atakaporejea. Hizi ni salamu za awali kwa niaba yenu wote na wote kwa kweli mliochangia kwenye jambo hili. Wengine kwa maombi yenu, wengine kwa kumtia moyo, kumpigia simu, wengine kwa kupiga simu kwa hao wapiga kura wa sehemu mbalimbali hapa barani Afrika. Tunawashukuru wote kwa namna mlivyoshiriki na pia tumemtaja Mheshimiwa Rais ni kwa niaba ya Serikali yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wote kwa kweli, Mawaziri wote, namna kila mmoja alivyoshiriki na Wabunge wenzetu pia wapo ambao walisafiri naye kwa ajili ya kwenda sehemu mbalimbali kutafuta kura na sasa ushindi umepatikana. Tunawashukuru sana pia upande wa Serikali kwa namna mnavyoyachukua haya mambo kwa uzito sana inapokuja kwenye kugombania hizi nafasi za kimataifa. Mambo mengi yanafanyika lakini kwa ujumla wake tunawashukuru sana Watanzania na tunawashukuru kwa sababu heshima hii tunaipata sisi sote kama Taifa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Maelezo ya Waziri wa Uchukuzi kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya Mwaka 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Rose Vicent Busiga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 21

### Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Nhomolwa – Mbogwe

**MHE. ROSE V. BUSIGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya, Kata ya Nhomolwa – Mbogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Nhomolwa kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe. Kituo hiki kilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi kwa kujenga jengo la kutolea huduma za nje *(OPD)* na majengo mawili ya wodi ya kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mbogwe ilipeleka shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje na nyumba ya mtumishi ya *two in one,* ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje umekamilika na kituo kimeanza kutoa huduma mwezi Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Mbogwe imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la maabara. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya Kituo cha Afya cha Nhomolwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ni lini Serikali Kuu itatenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo hicho cha Nhomolwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa huduma hizo zinazotolewa ni huduma ndogondogo kama vile upimaji wa watoto au upimaji wa malaria, ni lini sasa kituo hicho cha afya kitaenda kutoa huduma kulingana na hadhi ya vituo vya afya vingine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo ameendelea kufuatilia ujenzi wa Kituo hiki cha Afya cha Nhomolwa kwa manufaa ya wananchi wa Mbogwe. Nimhakikishie kwamba Serikali kupitia mapato ya ndani inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo yaliyobaki zikiwemo wodi, maabara na majengo mengine ili kituo kianze kutoa huduma zote za *level* ya kituo cha afya. Kwa Serikali Kuu mwaka 2025/2026, tutatenga fedha pia kwa ajili ya kuongeza

uwezo wa kukamilisha majengo haya kwa ajili ya kukamilisha kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na huduma zote za msingi za kituo cha afya zitaanza kutolewa mara majengo mengine yatakapokamilika ambayo yatatengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Hospitali ya Wilaya ya Itilima haina uzio je, ni lini Serikali itatuletea fedha za kujenga uzio? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Hospitali ya Halmashauri ya Itilima haina uzio, lakini ni moja ya hospitali ambazo Serikali imepeleka zaidi ya shilingi bilioni tatu na milioni mia tano kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali na sasa hospitali ile inatoa huduma. Sasa kwa sababu tumeshakamilisha hatua ya majengo tutaelekea sasa kuanza kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa uzio. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa, sasa aulize swali lake.

Na. 22

**Ujenzi wa Uzio wa Shule ya Wasichana Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha za ujenzi wa uzio wa Shule ya Wasichana Kondoa ili kuimarisha ulinzi na usalama wa wanafunzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021/2022 mpaka 2023/2024, Serikali Kuu imepeleka shilingi milioni 600.8 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo vyumba vya madarasa nane, mabweni mawili, matundu ya vyoo 14 na vitanda 660 katika Shule ya Wasichana Kondoa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uzio kwa ajili ya ulinzi wa mali na wanafunzi wa bweni. Hata hivyo, kwa sasa kipaumbele cha Serikali Kuu ni ujenzi wa miundombinu ya msingi inayowezesha kuongeza nafasi za udahili wa wanafunzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli aliyoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini shule ile ina uhitaji mkubwa wa hiyo *fence*. Naomba basi *commitment* ya Serikali kwa kuwa fensi hii ina umuhimu mkubwa; je, ni lini wanaweza wakaanza kufanya mpango wa kujenga *fence* hiyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na kabisa na Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze sana kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba wanafunzi katika shule hii ya wasichana wanaweza kupata usalama au wanaweza kupata ulinzi mzuri wanapokuwa katika mazingira ya shule. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kupitia mapato ya ndani katika mwaka wa fedha huu ujenzi wa fensi au uzio kwa hadhi ya matofali utaanza. Kwa hiyo, nimhakikishie Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa kuimarisha

usalama katika shule hii na itafanya jitihada kuhakikisha *fence* inakamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka pesa za kujenga uzio katika Sekondari ya Ubiri – Mlongwema na Shambalai ili kuimarisha ulinzi na usalama wa wanafunzi wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa ulinzi na usalama wa wanafunzi wetu wanapokuwa shuleni na Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi sana kuhakikisha inajenga miundombinu ya msingi ambayo itawezesha udahili wa wanafunzi ili waweze kuanza kusoma katika shule hizi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tayari Serikali imeanza awamu ya kwanza kuhakikisha inaweka majengo ya msingi. Serikali itatafuta na kutenga fedha ili kuhakikisha inaendelea kuimarisha miundombinu mingine ikiwemo ya uzio.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Wanandoa Waajiriwa kuwa Vituo vya Kazi vya Karibu**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza ustawi wa familia kwa kuweka wanandoa waajiriwa katika vituo vya kazi vya jirani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini ustawi wa familia ambao ni muhimu kwa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla. Ni kwa msingi huo, Serikali imeweka kipindi cha chini cha watumishi kukaa katika kituo kimoja cha kazi kabla ya kuhamishwa kuwa ni miaka mitatu na baada ya kipindi hicho kupita watumishi wanaweza kuwasilisha maombi ya uhamisho kwenda maeneo mengine kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuungana na wenza wao. Hata hivyo, maombi hayo yanapaswa kuzingatia uwepo wa mahitaji ya rasilimali watu kwa kada husika katika maeneo hayo. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya vibali vya uhamisho 8,846 vimetolewa vikiwemo vya watumishi wa kufuata wenza wao.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inafanya zoezi la tathmini ya mahitaji wa watumishi *(HR Assesment),* baada ya tathmini hii kukamilika Serikali itajua mahitaji halisi ya watumishi katika maeneo tofauti na kusaidia kufanya msawazo katika maeneo ambayo yatakuwa na upungufu, zoezi hili litasaidia kujaza nafasi katika maeneo yenye upungufu kwa kuzingatia hali ya ndoa. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa takwimu zinaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la ndoa nyingi zinazovunjika baada tu ya miaka miwili ya kufungwa kwake. Kufuatia takwa la Sheria za Ndoa la mwaka 1971, Serikali haioni haja ya kuondoa au kupunguza takwa hili au kigezo hiki cha miaka mitatu kwa waajiriwa wanaotafuta uhamisho kwa kigezo cha kufuata wenza wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa ni ukweli usiopingika kwamba malezi mazuri ya watoto na kuwepo kwa familia imara na bora kunategemea malezi ya wazazi wote wawili na sasa hivi nchini tumekuwa na changamoto kubwa sana ya mmomonyoko wa maadili kwa watoto. Hatuoni haja au Serikali haioni haja ya kuondoa kabisa kigezo hiki cha miaka mitatu kwa watu wanaotafuta uhamisho? Au kuwaweka moja kwa moja waajiriwa ambao ni wanandoa sehemu moja ya ajira? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kamani kwa namna ambavyo anafuatilia masuala ya haki za watumishi ikiwemo uhamisho.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali lake anasema kwamba kigezo cha miaka mitatu kuondolewa, Serikali iliweka kigezo hiki cha miaka mitatu kwanza ili kuweka *stability* ya taasisi, kwa maana ya kwamba ukiruhusu watumishi wakakaa kwa muda mfupi namna ya ku-*retain* na *performance* ya taasisi inaweza kushuka. Hii imeoneshwa katika Mikoa ya Pembezoni baada ya kuweka muda mfupi watumishi wengi wanachukua *check number* na kuondoka na baadaye kupelekea uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea kutoa vibali vya uhamisho kwa wale watumishi hasa wanaotaka kuungana na wenzao. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, maombi yalikuwa takribani 3,374 na Serikali imetoa vibali 1,136. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na jitihada hiyo bila kuathiri haki na maombi ya hawa watumishi wanaoomba kufuata wenza wao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni haja ya kuongeza kigezo cha 'mwenza wako' wakati wa kuomba ajira ili kuwarahisishia watumishi kuwapangia

mkoa ambao alikuwa anatoka mwenza wake na kuweza kupunguza gharama za kuhamisha watumishi hawa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetambua jambo hilo na ndiyo maana katika mwaka huu ajira zilizotangazwa 47,404, Serikali imewapa uhuru waombaji wa ajira hizo kuomba mikoa hiyo wanayotaka na lengo kubwa ni wao kwenda sehemu wanazotaka ili kuzuia wimbi hili la kuomba uhamisho kila wakati.  Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali. Kwenye halmashauri nyingi ambazo sisi tunakutananazo Kamati ya *LAAC* kumekuwa na watumishi wanaokaimu muda mrefu kiasi kwamba wanashindwa kufanya maamuzi sahihi kutokana na kukaimu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mnajaza nafasi kwenye halmashauri zote nchini ili kuwe na ufanisi na utendaji kazi ambao unaridhisha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, suala la kukaimu ni kweli limelalamikiwa na Serikali tumelichukua kwa uzito mkubwa. Hivi sasa kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tuna zoezi la kufanya *assessment* nchi nzima kuona wale watumishi wanaokaimu katika nafasi mbalimbali. Wale watakaokuwa wamekidhi vigezo, tayari Serikali imeandaa utaratibu wa kuwa-*confirm* na wale ambao watakua hawajakidhi vigezo basi utaratibu mwingine wa kujaza nafasi zile utafanyika. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Mradi wa *LNG* Nchini**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mipango gani wa kuharakisha Miradi ya *LNG* nchini ili kuchochea uchumi na kupunguza matumizi makubwa ya kuni na mkaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Kampuni za Nishati za Kimataifa *(International Energy Companies - IEC's)* kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(LNG)*. Aidha, Serikali inaendelea na kazi za awali ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa msingi wa kimazingira na kijamii, uelimishaji kwa wananchi juu ya umuhimu na manufaa ya mradi kupitia uhamasishaji wa matumizi ya gesi asilia kwa matumizi mbalimbali ikiwemo matumizi ya majumbani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na pia nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa nishati ya *LNG* ni nyenzo muhimu ya kiuchumi ili kuweza kuchochea uchumi wetu hali

kadhalika ni tiba sahihi ya mazingira yetu na hasa upoteaji wa misitu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatuambia kuna jitihada gani ambazo amezianzisha za kuweza kushirikiana na Sekta za Maliasili na Mazingira ili nazo ziwe katika utaratibu mzima huo wa mchakato wa uanzishaji wa matumizi ya gesi ya *LNG*?

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, kwa kuwa kuna ushirikiano mzuri katika matumizi ya *grid* ya Taifa ya umeme baina ya Tanzania Bara na Visiwani; Je, Mheshimiwa Waziri ameshaanza mchakato wa ushirikiano katika utaratibu mzima wa uanzishwaji au mchakato mzima wa *LNG* ili na Zanzibar nayo iweze kutumia fursa hii mara tu utaratibu utakapokamilika? Ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. Moja, ni kuhusiana na kushirikisha idara ya maliasili pamoja na mazingira. Suala la mazingira ni suala mtambuka, halihusishi sekta moja, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama anavyosema, wakati wote ambapo tunafanya majadiliano kuelekea utekelezaji wa mradi huu, sekta zote muhimu zinashirikishwa, kwa sababu ni kweli mradi huu unalenga kutuimarisha kiuchumi, lakini vilevile unalenga kuimarisha utunzaji wa mazingira. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sekta muhimu zote ambazo zinatakiwa kushirikishwa zinashirikishwa katika hatua zote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusiana na manufaa ya mradi huu kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa bado tupo katika hatua za majadiliano, lakini masuala yote yanayohusisha unufaika wa mradi huu yatazingatiwa pale ambapo mradi unakamilika na unaenda kutekelezwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera sasa aulize swali lake.

Na. 25

**Kodi kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Nchini**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuza:-

Je, lini Serikali itaondoa mzigo wa kodi kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama Nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa suala la ulinzi na usalama wa nchi, Serikali imekuwa ikitoa msamaha wa kodi kwa vyombo vya usalama na ulinzi ikiwemo misamaha inayotolewa kupitia Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, kwa mwaka 2024/2025, Serikali imefanya marekebisho kwenye Kipengele cha 18 cha Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha wa Kodi ili kujumuisha magari pamoja na vifaa vinavyotumiwa na vyombo vya ulinzi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, swali la nyongeza.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwamba wamefanya kazi nzuri ya kuliona hili. Je, Serikali sasa haioni haja ya kwenda mbali zaidi, kwa sababu hata nyuzi ya kiatu ya Askari bado ni silaha. Serikali haioni sasa kuwaachia vyombo vyetu vya ulinzi fursa kamili ya kuwa na msamaha? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ushauri wake umepokelewa, kwa sababu amesema huoni haja ya kutanua wigo. Tumepokea ushauri huo na tutaufanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa nchi hii ili ufanye biashara unahitaji *tax clearance* na *tax clearance* inahusisha ulipaji wa kodi. Je, ni kwa nini Serikali isiainishe aina za biashara ambazo unaweza kupata leseni bila kuwa na *tax clearance* mpaka u-*run* biashara kwa muda fulani ili uweze ku-*file* na kulipa kodi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, samahani sijamwelewa kidogo maana yake ametoka nje ya hii mada naomba arudie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwanza zungumza Kiswahili ama zungumza Kiingereza maana hiyo nayo unatuchanganya. Haya uliza swali lako upya.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sijui t*ax clearance* inaitwaje kwa Kiswahili lakini kwa biashara nyingi...

**SPIKA:** Basi zungumza Kiingereza kwa sababu Kanuni zinaruhusu. Uliza swali lako kwa Kiingereza. *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, aah! Kwa Kiingereza? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima...

**SPIKA:** Haya ngoja nimweleweshe swali lako. Mheshimiwa Mbunge anasema hivi, mtu anapoenda kuomba leseni ya biashara, inataka awe ni kama vile alishakuwa mlipakodi kabla, yaani apate kile cheti kinachoonesha kwamba yeye hadaiwi kodi; kitu kama hicho. Sasa hicho cheti ndiyo jina lake kwa Kiswahili amepata changamoto, lakini anataka kujua kwa nini anaombwa kabla, si apewe ili aanze biashara. Kwa nini anaombwa kabla? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida *tax clearance* hutolewa, aah! Kiingereza. Cheti kile hutolewa baada ya biashara na Serikali inasema kwamba, mtu aanze kufanya biashara kwanza ndiyo anaenda kuomba hicho cheti cha ruhusa ya kufanyia biashara. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa hoja yake si ni kwamba, hiyo biashara hawezi kuanza bila leseni? Yaani ni kwamba yale maombi ya leseni ili biashara yake afanye kwa utaratibu wa kisheria, unataka hiki cheti kwanza, ndiyo swali lake liko hapo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka jana tulijibu swali kama hili na tukatoa maelekezo kwa *Commissioner General* wa *TRA* kwamba, yeyote ambaye ameanzisha biashara, lakini biashara ile bado haijafanya kazi na faida yake kuonekana, apewe cheti hicho ili aende akapate leseni ya kufanya biashara. Asiwe na kikwazo kwa sababu hajapata hiyo *tax clearance*.

**SPIKA:** Haya. Nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Mtaalam wa Kiswahili humu ndani. Yupo, si Mheshimiwa Almas Maige? Mheshimiwa, *tax clearance* inaitwa nini Kiswahili?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, *tax clearance* inaweza ikatoholewa kama *tax clearance* lakini ni cheti cha... *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya sawa, hiyo imeeleweka. Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Malipo ya Katikati ya Mwezi kwa Wastaafu**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza:-

Je, ni muda gani Hazina hulipa malipo ya katikati ya mwezi kwa Wastaafu kwa Mfuko ulioanza mwaka 1992 kwa kuwa hawalipwi kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha inahusika kulipa michango ya mwajiri kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(PSSSF, ZSSF, WCF* na *NHIF)* kila mwezi pamoja na malipo ya nyongeza ya pensheni. Aidha, Wizara ya Fedha hulipa pensheni za kila mwezi pamoja na mafao ya hitimisho kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali na nimefuatilia ndiyo inavyokuwa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali ilifanya utaratibu mzuri wa kurekebisha kile kikokotoo, lakini kuna wastaafu ambao walituahidi kwamba wale ambao waliathirika na kikokotoo basi ile sehemu yao ambayo ilikuwa imeathirika kwa marekebisho mapya watawalipa, je, wataanza kuwalipa lini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni hili; kwanza na-*declare interest* kwamba nilikuwa ni mdau au ni mhanga kwenye

jambo hili ninalokwenda kuliuliza. Tuna changamoto kubwa ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini ambapo fedha zao na vifaa vyao vilichukuliwa na Serikali iliahidi kurudisha, lakini mpaka sasa baadhi bado hawajarudishiwa zile fedha na vifaa vyao. Naomba kujua, Serikali itarudisha lini?

Mheshimiwa Spika, nisiporidhika na majibu yake, nitakuomba ule utaratibu uliotumia jana kwenye lile Shamba la Rukwa, utumike pia na hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ngoja, ngoja Mheshimiwa! Sasa hapo Mheshimiwa Naibu Waziri hatojua ajibu kipi sasa, maana hapo una vitu vitatu kwa wakati mmoja. Mpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu maswali uliyouliza. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Msambatavangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, baada tu ya taratibu kukamilika na wale waathirika wa suala hili la kikokotoo watafanikiwa na wao kupata stahiki zao kama ilivyopangwa ambavyo watapata wale wengine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu maduka ambayo yalifungwa na Serikali kuahidi kurejesha fedha hizo, maduka haya yalikuwa jumla ni 67 na tayari 62 Serikali imesharejesha vifaa na fedha yao. Bado maduka matano akiwemo na dada yangu Msambatavangu, lakini nimhakikishie kwamba na haya matano yaliyobaki tutafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ameuliza *specific* na yeye mwenyewe, naomba uniruhusu baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu nikae naye kama Kamati tujadili suala hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa John Denielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Matawi ya Benki – Kikatiti**

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuelekeza Benki za *CRDB*, *NBC* na *NMB* kufungua Matawi eneo la Kikatiti linalokua kwa kasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kufungua tawi jipya la benki, benki husika hufanya upembuzi yakinifu kwa lengo la kujiridhisha kama kuna fursa za kibiashara kukidhi gharama za uendeshaji na kutengeneza faida. Upembuzi huo, pamoja na mambo mengine, huiwezesha benki husika kufanya maamuzi ya kufungua tawi katika eneo husika. Aidha, jukumu la Serikali ni kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ikiwemo huduma ya ulinzi na usalama, miundombinu ya barabara, nishati, maji na TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba *CRDB, NBC* na *NMB* hazina matawi Kikatiti, wananchi wa eneo hilo wanaendelea kupata huduma za kibenki kupitia kwa mawakala. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; eneo hili la Kikatiti liko Tarafa ya King'ori ambayo ina Kata 10 zenye watu 124,000, pia eneo hilo ndilo kapu la chakula kwa Jiji la Arusha na viunga vyake. Kikatiti yenyewe ina watu .....

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni je, kwa takwimu ambazo zipo katika Sensa ya Mwaka 2022, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka benki hizi zifungue matawi pale?

Mheshimiwa Spika, kama ni ngumu sana, ni kwa nini benki hizi zisifungue mashine za kutolea fedha *(ATM's)* Eneo la Maji ya Chai, Kikatiti yenyewe na King'ori Madukani? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Pallangyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu aliyotaja ni kweli inaleta ushawishi kufungua tawi la benki huko, lakini jukumu la Serikali kama nilivyojibu ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji. Kwa hiyo, naomba tu Benki za *NMB, CRDB* na nyingine waende kuangalia hiyo fursa ili ikiwezekana wafungue tawi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni ushauri, naomba tuchukue na tunaenda kuufanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 28

**Hatua za Kunusuru Theluji Mlima Kilimanjaro**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za muda mfupi wa kati na muda mrefu kunusuru theluji inayotoweka Mlima Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kupungua kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro ni kuongezeka kwa joto la dunia kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayochangiwa na ongezeko la shughuli za kibinadamu hususan ukataji wa miti, kilimo, uchomaji wa moto katika maeneo yanayozunguka mlima, uwepo wa mvua chache na vipindi vya ukame na upepo mkavu kutoka Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mikakati ya muda mfupi Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanga kupanda miti takriban milioni nane kwa mwaka katika Mkoa wa Kilimanjaro, sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu upandaji miti na uhifadhi wa mazingira kupitia vipindi vya redio, televisheni, matamasha na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau imezindua kampeni ya kupanda miti zaidi ya bilioni moja katika Mikoa ya Kaskazini ili kunusuru barafu ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya muda wa kati ni pamoja na kuhimiza matumizi bora ya ardhi na kuimarisha ulinzi katika maeneo yanayozunguka Mlima Kilimanjaro na kutekeleza mipango ya kudhibiti na kupambana na uchomaji moto mlimani. Aidha, katika kutekeleza mikakati ya muda mrefu, Serikali inaendelea kushirikiana na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kutekeleza mikakati ya pamoja ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kuboresha teknolojia za kilimo, kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji, kupunguza

uzalishaji wa gesi chafu na kurejesha mifumo ya ikolojia kwenye mlima na maeneo yanayozunguka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Nina maswali mawili ya kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la kwanza; Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro ni wadau muhimu sana wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwashirikisha Wabunge hawa kwenye hii programu ya kupanda miti ili hili zoezi liweze kufanikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tafiti nyingi zinazofanywa hapa nchini kuhusiana na Mlima Kilimanjaro, zinafanywa na watafiti kutoka nje ya Tanzania. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwashirikisha watafiti wazawa na kuwawezesha ili waweze kushiriki kwenye kuulinda huu mlima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, siku zote wamekuwa ni wadau muhimu katika kushajihisha shughuli za kimaendeleo katika nchi yetu. Kwa hiyo, Wizara tuko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro katika upandaji wa miti. Taasisi yetu ya Hifadhi ya Kilimanjaro ina mpango wa kutoa miche kwa watu ili waweze kuipanda nje ya maeneo ya Mlima Kilimanjaro. Kwa hiyo, tuko tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge na kuwapatia miche hiyo, nitaomba leo mchana tukutane na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro ili tuweze kuainisha mahitaji yao na tuweze kuona jinsi ambavyo tunaweza kushirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la tafiti, ni kweli kwamba zipo tafiti zaidi ya tano ambazo zimefanywa na watafiti

kutoka nje, lakini wakati wote walipofanya tafiti hizi walishirikisha watafiti wa Kitanzania, lakini kwa sababu tunafahamu kwamba suala la mabadiliko ya tabianchi ni suala mtambuka, taasisi zetu sasa za hapa nchini kama *SUA*, *University of Dar es Salaam*, *UDOM*, Nelson Mandela na nyinginezo zimeshiriki kikamilifu katika kufanya tafiti zinazoendana na kupata afua zitakazosaidia kwenye mabadiliko ya tabianchi. Ni imani yetu kwamba tafiti hizi zitatusaidia sana kama nchi kuwa na uelewa mpana wa tatizo tunalokabiliana nalo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, nilikuona lakini pia Mheshimiwa Shally Raymond. Maadam Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mna kikao mchana huu, naamini mtapata nafasi ya kuyazungumza huko Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 29

**Ujenzi wa Jengo la Mahakama – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Meatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo

mapya na ya kisasa na kukarabati majengo chakavu. Wilaya ya Meatu ni moja ya wilaya ambazo zina majengo ya Mahakama lakini jengo lake ni chakavu na siyo la kisasa. Kwa mujibu wa mpango wa ujenzi wa majengo ya Mahakama, Wilaya ya Meatu itajengewa jengo la kisasa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Mahakama ya Mwanzo iliyopo Kata ya Bukundi katika Tarafa ya Nyalanja jengo lake ni chakavu sana la miaka 60. Je, Serikali haioni haja ya kutuweka kwenye mpango wa kutujengea jengo jipya au kutufanyia ukarabati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya kwa kufuatilia kwa karibu sana ujenzi wa Mahakama katika Jimbo lake la Meatu ili wananchi wa Meatu wapate haki yao kwa ukaribu na kwa ufanisi zaidi. Nalichukua suala hilo la Mahakama ya Bukundi nalo tutaliingiza katika mpango wa ukarabati au ujenzi mpya wa Mahakama katika mwaka wa 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wananchi wa eneo la Nkaiti, Wilayani Babati wamekuwa wakifuata huduma za Mahakama kwa umbali mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kujenga Mahakama ya Mwanzo katika eneo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kulichukua swali hilo ili tuweze kulifanyia kazi na wenyewe pia waweze kuingizwa katika ujenzi wa Mahakama katika mwaka ujao wa fedha ili kuwafikishia huduma muhimu za upataji wa haki.

**SPIKA:** Mheshimiwa; kati yenu nani amewahi kufika Bungeni leo, nani ametangulia kuingia Bungeni leo kati yenu? Mheshimiwa Stella Fiyao swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nataka kujua mpango wa Serikali kujenga Mahakama nzuri na ya kisasa katika Wilaya ya Momba ili kuepukana na changamoto za kupangapanga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Momba ni moja ya wilaya ambazo zipo katika mpango wa ujenzi wa Mahakama mpya za wilaya na mara ya taratibu zote zitakapokuwa zimekamilika za upatikanaji wa fedha, basi Mahakama hiyo itajengwa katika Wilaya ya Momba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge nimeuliza hivyo kwa sababu nimewaona wote kwa pamoja sasa nikawa nataka kujua nimwite yupi katika yao, kwa hiyo ikabidi nitumie kigezo cha ziada.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 30

**Ushindani wa Ununuzi wa Zao la Pamba Nchini**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuna ushindani miongoni mwa wafanyabiashara wanunuzi wa zao la pamba nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mifumo ya ununuzi na kuhakikisha kunakuwa na ushindani katika ununuzi wa pamba kwa mujibu wa sheria na miongozo ya biashara ya zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa pamba nchini hufanyika kwa utaratibu wa soko huru ambapo zaidi ya kampuni 35 zimesajiliwa na kupewa leseni ya kununua pamba na usajili unaendelea ili kuongeza ushindani. Kampuni hizi hununua pamba kulingana na hali ya soko ya msimu husika na bei dira iliyokubaliwa na wadau. Aidha, Serikali husimamia na kuhakikisha bei dira iliyokubalika na wadau inazingatiwa katika ununuzi wa pamba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kampuni hizi zinapofika ngazi ya wilaya au kata yanagawanywa kwenye kata moja, mbili au tatu na hivyo kutengeneza ukiritimba kwenye hilo eneo. Yaani kampuni moja inanunua pamba kwenye hilo eneo na kufifisha sasa ushindani ambao tuliutarajia. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na tabia ya namna hii? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, moja ni kwamba wanunuzi wote wenye leseni wanaruhusiwa kununua pamba eneo lolote isipokuwa katika kesi ambayo anaeleza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kulikuwa na kampuni ambazo zilielekeza katika kata kama 40 kama *case study* ili kuweza kujifunza namna ambavyo wamefanya uwekezaji katika pamba ikiwemo kutoa pembejeo kwa wakulima wa pamba. Kwa hiyo wakaruhusiwa vilevile kununua katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tamko la Serikali ni kwamba, maeneo yote ambayo wanunuzi wote wamepewa leseni wana haki sawa ya kununua pamba. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla Mbunge wa Ulyankulu swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 31

**Wakulima wa Tumbaku Kukopeshwa Pembejeo na Kuuza Tumbaku kwa Dola**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, ni sababu zipi zinasababisha wakulima wa tumbaku kukopeshwa pembejeo na kuuza tumbaku kwa Dola badala ya shilingi ya Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Utaratibu wa wakulima wa tumbaku kukopeshwa pembejeo na kuuza tumbaku kwa Dola za Marekani na kulipwa kwa dola unatokana sababu za msingi zifuatazo:-

(i) Biashara ya tumbaku Kimataifa hufanyika kwa Dola za Kimarekani kuanzia upatikanaji wa pembejeo, ugharamiaji wa uzalishaji hadi uuzaji;

(ii) Uuzaji wa tumbaku kwa Dola za Kimarekani unamlinda mkulima na hasara ambazo zinatokana na mabadiliko ya shilingi na kumhakikishia uimara wa kipato chake;

(iii) Zao la Tumbaku linaendeshwa katika misingi ya kibiashara ya mikataba inayosimamia ubora, madaraja na taratibu zake hadi inapofikishwa katika soko na hupimwa kwa viwango vya Kimataifa; na

(iv) Mfumo huu unaihakikishia nchi upatikanaji wa dola za Kimarekani na usimamizi rahisi wa fedha za mauzo kurudi ndani ya nchi. Mfano, msimu wa Mwaka wa Fedha 2022/2023, wakulima wa tumbaku walilipwa Dola za Kimarekani milioni 286.8 na Taifa letu lilipata Dola za Kimarekani milioni 480 kutokana na kuzalisha na kuuza tani 122.8 za tumbaku nje ya nchi na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya pili kwa Afrika katika uzalishaji na mauzo ya tumbaku nje ya nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kwa vile biashara yote ya tumbaku inalipwa kwa dola, kwa nini wakulima wanalipwa kwa shilingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tumbaku inafanyika kwa dola na kinachofanyika ni kwamba *transaction* inapotoka kwa mnunuzi kwenda kwenye vyama vikuu vya msingi huwa vinafanyika kwa dola. Inapotoka kwenye *transaction* kutoka katika vyama vya msingi baada ya makato yote ambayo wakulima wanakuwa walikopa katika msimu wa kilimo, ile *difference* inayobaki wakulima wanalipwa kwa shilingi kulingana

na thamani ya fedha ya siku hiyo husika. Hicho ndicho ambacho kinafanyika sasa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Sasa huyo anayebadilishia hapo katikati ni nani kama mkulima huwa anapata pembejeo kwa dola na yule mnunuzi ananunua kwa dola, nani anayembadilishia mkulima hapo ghafla kwamba yeye ndiyo apewe shilingi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni Chama Kikuu cha Msingi *(TCJE)* ambao sasa wao ndiyo wameingia mikataba na wakulima kwa sababu zile *account* za wakulima ni za shilingi. Kwa hiyo wao wanachokifanya wana-*convert* ile thamani ya dola ya siku hiyo; yaani kwa mfano labda mkulima thamani yake labda ni dola 100 kwa hiyo wanakwenda kuangalia katika thamani ya bei ya shilingi ya dola kwa siku hiyo kama ni 2,500, kwa hiyo watalipwa ile shilingi 250,000/=, lakini hiyo inatoka kwenye Chama cha Msingi, Chama Kikuu cha Ushirika kwenda kwa mkulima.

**SPIKA:** Lile katazo alilosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati wa Bunge la Bajeti sina uhakika kama tuliingiza kwenye *Finance Act* ama hapana lakini si lilitoka katazo hapa kuhusu matumizi ya dola ili tuweze kulinda shilingi yetu isiporomoke? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, ametoka kidogo. Nafikiri lilitoka tangazo hapa au ni mimi peke yangu nakumbuka?

Lilitoka katazo kwamba yaani mauziano haya, mauziano na manunuzi ya dola hapa nchini yaondolewe ili kuondoa hili. Sasa hapa mbona jibu lenu Serikali linaonyesha tena na ninyi mnatia moyo yaani kwamba ndivyo ambavyo inatakiwa?

Haya tumekusikia Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kafuatilieni katazo lenu wenyewe na haya majibu ambayo leo mmeyaleta yanayohusu kukopeshwa mkulima dola na kuuza kwa dola halafu yeye inageukia katikati hapo anajikuta kwamba amepata tena shilingi.

Kwa hiyo nyinyi mlileta katazo hapa ndani labda kama lile katazo sikumbuki vizuri kama tuliliweka kwenye Sheria ama

Hapana, kama tuliliweka kwenye Sheria yatakuwa ni makosa haya. Yaani haya majibu yatakuwa ni makosa kwa swali la Mheshimiwa Mbunge, lakini kama hatukuweka kwenye Sheria ni jambo la kuanza kulifikiri sasa.

Haya Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza, Mheshimiwa subiri kidogo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua kwa kuwa Mkoa wa Mara, Wilaya ya Serengeti imekuwa ikilima zao la tumbaku sana na sisi Jimbo la Bunda kuna maeneo yanayofanana na Serengeti. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka wataalam wa kupima ule udongo wa Jimbo la Bunda ili waweze kulima zao la tumbaku? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge Mwita Getere kwamba mara baada ya Bunge letu la mchana nitakwenda kuzungumza na wataalam ili tuweze kutuma wataalam katika eneo lake waweze kupima na kuona kama linafaa. Kwa hiyo tutalifanya hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 32

**Hitaji la Kiwanja cha Michezo – Njombe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kiwanja cha michezo cha Kisasa Mkoani Njombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ipo kwenye ukarabati wa viwanja vya Uhuru na Benjamin Mkapa, ujenzi wa uwanja wa Arusha *(Arusha Stadium)* na kukarabati viwanja vingine vitano (5) vya mazoezi kwa ajili ya mashindano ya *CHAN* 2024 na *AFCON* 2027. Kama sera ya michezo inavyoelekeza, ujenzi wa miundombinu ya michezo ikiwemo viwanja ni jukumu la Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Baada ya kukamilisha ujenzi wa viwanja kwa ajili ya mashindano ya *CHAN* 2024 na *AFCON* 2027, Serikali itatoa maelekezo kwa uongozi wa Mikoa yote ili kutekeleza mkakati wa ujenzi wa miundombinu ya michezo katika Mikoa yote. nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na naipongeza sana Serikali kwa utaratibu wa kupata na kufanyisha mashindano ya *AFCON* 2025 na 2027. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, sielewi ni kwa nini Wizara kwa mikoa ambayo haipo kwenye *AFCON* watoe maelekezo baada ya michezo ya *AFCON* kufanyika au ujenzi wa viwanja vya *AFCON* kufanyika 2027. Nadhani kwamba wangeweza wakatoa maelekezo sasa hivi ili mikoa mingine na yenyewe iweze kuwa na mikakati ya kujenga viwanja hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa michezo siyo afya tu na michezo siyo ajira tu, michezo katika ulimwengu wa sasa ni utalii. Serikali kupitia Wizara hii ina mkakati gani kwa kushirikiana na Wizara nyingine kuhakikisha sasa michezo kwenye maeneo yenye hali ya hewa nzuri kama Njombe inaleta michezo ya kiutalii kama *golf?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Mwanyika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge ameliona sahihi. Ipo haja ya kuharakisha utaratibu wa kuzielekeza mamlaka za mikoa ambayo haitachezewa *AFCON* kuanza ujenzi wa miundombinu bora ya michezo hasa ile mikoa ambayo haina viwanja hivi. Kwa hiyo tumelichukua tutalifanyia kazi atupe muda.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili, tumeshaanza mikakati ya kuunganisha utalii na michezo kwenye hili la utalii wa kimichezo hasa wa *golf*. Moja ya mambo ambayo tumeyafanya sasa hivi, ni kufufua viwanja vya zamani ambavyo vilikuwa vimekufa (vimeuliwa). Kwa mfano pale Njombe kulikuwa na kiwanja kilikuwa na mashimo tisa cha *golf* cha kwenye *Kibena Tea Estate* na tumeanza utaratibu wa kukifufua. Moshi pia kulikuwa na uwanja pia wa mwaka 1922 wa *golf* ambao nao umekufa na tumeshaanza kuufanyia kazi ambapo Mheshimiwa Waziri alimpa maelekezo Mtendaji Mkuu wa *BMT* na uwanja ule umeshaanza kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, tutakapomaliza kukarabati na kuvifungua viwanja hivi, jambo la kwanza tutakalofanya ni kuandaa mashindano mbalimbali ya Kitaifa na ya Kimataifa ya *golf* ili kuhakikisha kwamba tunaunganisha utalii na michezo kwa kutumia mchezo wa *golf*. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa *memorial* kama walivyoahidi katika kipindi cha mashindano ya *Kilimanjaro Marathon* ili uweze kutumika kama kambi katika mashindano ya *AFCON*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu mwanzoni viwanja vyote ambavyo vitatumika kwa ajili ya *AFCON* ujenzi umeshaanza na vile ambavyo vitatumika kama sehemu ya viwanja vya

mazoezi ujenzi wake utaanza hivi karibuni. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Serikali ilishaahidi kuanza kukikarabati kiwanja cha *memorial*, ukarabati huo utaanza hivi karibuni na asiwe na wasiwasi akae kwa kutulia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma swali la yongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ipo tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya Hanang ili kujenga uwanja wa kisasa wa michezo pale Hanang ambapo eneo tayari limetengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu wakati najibu swali la msingi kwa sasa msisitizo upo kwenye viwanja ambavyo vitatumika kwa ajili ya mashindano ya *AFCON*. Pia kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Deodatus Mwanyika aliuliza kama kwa nini tunasubiri mpaka *AFCON* ipite ndiyo tuzielekeze mamlaka za mikoa kuanza kutengeneza miundombinu ya michezo kwenye maeneo yao. Nimeahidi na inamuahidi tena Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutauharakisha utaratibu huo ili mamlaka za mikoa na wilaya zianze kufanya ujenzi huu wa miundombinu ya michezo kwenye maeneo husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 33

**Kukabiliana na Vitendo vya Ukatili kwa Wanawake na Watoto Nchini**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa Serikali kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini hasa kwa wanawake na watoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Baadhi ya mikakati inayotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Ulinzi na Usalama wa Mtoto umewasilishwa Bungeni na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza;

(ii) Mpango kazi wa Taifa wa Awamu ya Pili wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II) umezinduliwa Mei, 2024;

(iii) Elimu kwa umma imeimarishwa kwa ushirikiano na Maafisa Polisi ngazi ya Kata. Pia, kimeanzishwa Kituo cha Huduma kwa Wateja Wizarani *(Call Centre)* ili kuongeza nguvu ya elimu kwa umma na kupokea taarifa za vitendo vya ukatili;

(iv) Huduma za madawati ya Jinsia na Watoto zinapatikana katika vituo vyote vya Jeshi la Polisi. Pia, idadi ya Vituo vya huduma ya dharura na jumuishi kwa manusura wa ukatili imeongezeka na kufikia vituo 26 nchini;

(v) Aidha, programu ya elimu ya malezi na makuzi chanya ya maendeleo ya awali ya mtoto inatekelezwa kwenye mikoa na halmashauri zote nchini na pia; na

(vi) Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipata kibali cha ajira kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 800 na Maafisa Ustawi wa Jamii 350.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini kadri siku zinavyokwenda vitendo hivi vya ukatili vinazidi kuongezeka siku hadi siku nchini nchini na kumekuwa na mikakati mingi, mipango mingi, lakini bado vitendo hivi vinaongezeka kwa kasi. Je, ni upi mpango wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na mpango wa maendeleo ya Wizara ya Mambo ya Ndani upi mpango jumuishi wa kuhakikisha wanapambana na vitendo hivi vya ukatili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, ni lini sasa vitendo hivi vitakoma? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la mwanzo, Mpango jumuishi unaohusisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni dawati la watoto la kijinsia, lakini pia Polisi ni moja ya Kamati ya Kudumu ya Kutokomeza Ukatili wa Wanawake na Watoto ambapo tunashirikiana pamoja kuwa kuhakikisha MTAKUWWA unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, 60% ya vitendo vya ukatili vinatokana na jamii. Kwa hiyo niwaombe wananchi au Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane kwa pamoja, tukiona ishara ya vitendo vya ukatili basi tushirikiane na kamati za kisekta; tutashirikiana ili kuhakikisha kwamba vitendo hivyo vinachukuliwa hatua mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Shengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ni Mnzava.

**SPIKA:** Samahani, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vitendo hivi vinakithiri kila siku na sheria iliyopo ni ya kifungo cha Maisha. Je, Wizara hawaoni kwamba kuna umuhimu wa kuleta Muswada ili kubadilisha kutoka kifungo cha maisha na kuwa adhabu ya kifo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vitendo hivi tunajua vimekithiri katika nchi yetu na Wizara hivi sasa imeleta Muswada wa Sheria kuhakikisha tunarekebisha sheria hizo na kuhakikisha kwamba wale wote wanaohusika na vitendo hivi vya ukatili basi hatua kali zinachukuliwa dhidi yao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 34

**Hitaji la Magari ya Polisi – Morogoro**

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka magari Vituo vya Polisi Kisaki na Mvuha ili kukabiliana na migogoro ya Wakulima na Wafugaji na kulinda raia na mali zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Kisaki kina gari moja *PT 4770 Ashok Leyland* na Kituo cha Polisi cha Mvuha hakina gari kwa sasa na kinahudumiwa na Kituo Kikuu cha Wilaya pamoja na Kisaki. Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali imenunua magari 122 kwa ajili ya Wakuu wa Polisi wa Wilaya na magari hayo yanatarajiwa kuwasili nchini wakati wowote kuanzia sasa. Katika mgao wa magari hayo Wilaya ya Morogoro imetengewa gari ambalo pia litatumika kudhibiti uhalifu maeneo ya Tarafa ya Mvuha. Serikali itaendelea kutenga fedha toka kwenye bajeti yake kila mwaka kwa ajili ya kununulia vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi ikiwemo magari ili kudhibiti uhalifu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALEGORIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, nini kauli ya Serikali katika hili suala la gari ambalo limetengewa Wilaya ya Morogoro ambalo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba litatumika katika kutoa huduma katika Tarafa ya Mvuha. Nataka nipate *commitment* ya Serikali kumwelekeza *OCD* wa Morogoro gari hilo litakapokuwa limefika liende katika Kituo cha Tarafa ya Mvuha ili liweze kuhudumia Tarafa nne ambazo ni Ngerengere, Matombo, Mkuyuni na Mvuha yenyewe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Morogoro Vijijini imetenga kiasi cha shilingi milioni mia tatu ambazo zimejenga jengo la Kituo cha Polisi chenye hadhi ya wilaya. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha jengo hili ambalo linahitaji shilingi milioni mia moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBI WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza, magari tuliyoyaagiza kwa sasa ni magari ya Ma-*OCD* ambao wapo kwenye Wilaya za Kipolisi, kwa hiyo gari hili litakalokuja litahudumia Wilaya nzima ya Morogoro kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jengo ambalo limejengwa na wananchi, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa aliyofanya ya kujenga jengo la Polisi. Nimhakikishie kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kumalizia maboma ambayo wananchi wameyajenga kwa nguvu zao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 35

**Ukarabati wa Nyumba za Polisi – Kaskazini Pemba**

**MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati nyumba za makazi ya Polisi zilizopo Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi 100,000,000 kutoka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kwa ajili ya kufanya ukarabati nyumba ya makazi ya Askari Polisi ya familia 12. Aidha, tathmini kwa ajili ya

ukarabati wa nyumba nane za makazi ya kuishi familia 32 za askari Polisi imeshafanyika na kiasi cha fedha shilingi 416,000,000 zinahitajika. Fedha kwa ajili ya ukarabati zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali na Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharif Omar, swali la nyongeza.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri lakini bado kuna mahitaji makubwa ya kupata makazi ya kudumu katika maeneo ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ili kuondosha usumbufu. Swali la kwanza; ningependa kujua, je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuandaa makazi kwa askari wetu hao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza maeneo ya makazi katika Wilaya ya Wete ili kuondosha askari wetu kupanga nyumba za mitaani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Asya Sharif, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza, kwamba kuna mahitaji makubwa ya makazi, ni kweli na sisi kama Serikali tunatambua kuwa kuna mahitaji makubwa ya makazi ya askari wetu. Tunatenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha kwamba tunakarabati na kujenga makazi ya askari wetu ili wafanye kazi ya kulinda wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la maeneo ya makazi, Serikali itafanya tathmini katika maeneo yote ya Pemba na kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yanafaa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya askari yatatengewa bajeti katika miaka inayokuja ya fedha, 2025/2026 na miaka inayoendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

Na. 36

**Zabuni za Ujenzi wa Barabara ya Mbambo – Ntaba hadi Ipinda – Mbeya**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE K.n.y. MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, lini zabuni ya ujenzi wa Barabara ya Mbambo – Ntaba hadi Ipinda kwa kiwango cha lami itatangazwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mbambo – Ntaba hadi Ipinda yenye urefu wa kilometa 18.13. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Barabara ya Katumba – Mwakaleli – Ruangwa – Mbambo hadi Tukuyu imeshampata mkandarasi lakini sasa hivi ni zaidi ya miezi sita bado mkandarasi hajalipwa *advance* ili kuanza kazi. Je, ni lini atalipwa ili aanze kazi kwenye barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya Mrishaka – Nkwenda – Mulongo Wilayani Kyerwa imempata mkandarasi zaidi ya miezi nane, mpaka sasa hivi bado hajalipwa *advance* ili kuanza kazi, je, ni lini atalipwa ili kazi ianze?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Barabara ya Katumba – Mwakaleli – Mbambo imeshampata mkandarasi na ni kweli kwamba tumeshasaini mkataba. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi tunachofanya ni maandalizi ya kumlipa fedha za awali ili mkandarasi huyu aanze kufanya kazi hiyo ya kuanza ujenzi. Hata hivyo tunamhimiza mkandarasi aendelee kufanya maandalizi ya awali kwa mujibu wa mkataba unavyomtaka.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, swali lake la pili linafanana na hilo suala la kwanza kwa Barabara ya Mrishaka kwenda Kyerwa ambayo pia mkandarasi ameshasaini. Sisi kama Wizara tumeshawasilisha maombi ya *advance* ya mkandarasi huyu, kwa maana ya fedha za awali ili aweze kulipwa na mkandarasi huyo aweze kuanza kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mwaka jana mwezi Juni tulisaini miktaba kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Nachingwea – Masasi mpaka Liwale na sasa hivi ni mwaka mzima, kazi hiyo haijafanyika. Nataka kufahamu, ni lini hasa ujenzi wa barabara hii utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, alichosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, lakini swali hili jana tulilijibu lilikuwa kama swali la msingi. Tulieleza kwamba barabara hii ilikuwa imesainiwa kwa kutumia utaratibu wa *EPC+ F* na tukasema Serikali inapitia upya utaratibu huo wa ujenzi kulingana na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa utaratibu huo. Tayari tunafanya mapitio na tutakuja kutoa taarifa kamili kuhusu utaratibu ambao tunaona utakuwa ni bora ili tuendane na kasi ya kuanza kujenga barabara hizo, ikiwezekana kwa utaratibu mpya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Aprili, 2019, Mheshimiwa Rais aliagiza barabara ya Ipanda – Mbambo kilomita 19 ianze kujengwa mara moja. Je, ni kwa nini Serikali inasitasita na kutokuipa kipaumbele mpaka sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haisitisiti na maagizo ya viongozi wa kitaifa huwa ni maelekezo ambayo lazima Serikali itekeleze. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tunaendelea kutafuta fedha ili kipande hiki cha Ipinda – Mbambo kiweze kujengwa kama alivyokuwa ameagiza Mheshimiwa Rais. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je, ni lini sasa Wizara ya Ujenzi itatoa tarehe isiyo ya kufikirika juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park* ikipita Kalenga na kwa Mheshimiwa Lukuvi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe *comfort* Mheshimiwa Mbunge, kwamba hizi barabara zinafadhiliwa na wenzetu wa *World Bank* kwenye mpango

tunaouita *TANTIP*. Tayari barabara zilishatangazwa na sasa hivi tuko kwenye *valuations* ambazo tunategemea kwamba kabla ya mwisho wa Septemba miradi hiyo yote; ipo kama miradi mitano; itasainiwa mwezi huu wa Septemba tunaouendea sasa hivi ili barabara pamoja na viwanja vya ndege vianze kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, Bunge lililopita la Bajeti Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba wanakwenda kumtafuta mshauri elekezi kwa ajili ya Barabara yetu ya kutoka Kahama – Nyang'hwale – Busisi kwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, huyu mshauri elekezi anaanza lini kazi hiyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, taarifa nilizonazo ni kwamba mshauri wa barabara hiyo ambayo inaunganisha Mkoa wa Geita, Mwanza na Shinyanga atasaini mkataba mwezi Septemba mwaka huu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ni lini zoezi la upembuzi yakinifu kwenye Barabara ya Mtama – Kitangali – Newala utakamilika ili ujenzi kwa kiwango cha lami uanze kwenye barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, upembuzi na usanifu wa kina unategemea mkataba wenyewe na kazi yenyewe ilivyo. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunategemea utakamilika kwa mujibu wa mkataba. Kama kutatokea changamoto zozote ama kama kuna changamoto zozote Mheshimiwa Mbunge ameziona, basi

tuwasiliane ili tuweze kuzitatua, lakini tunategemea utatekelezwa na kutimizwa kwa mujibu wa mkataba. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge ambao mko viti vya Mawaziri, uzuri mimi ni mwalimu, kwa hiyo sitochoka kufundisha. Mpishe sasa hivi kipindi cha maswali kiishe ili waweze kusikiliza maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani.

Na. 37

**Ujenzi wa Barabara ya Nhungumalwa - Ngudu mpaka Magu**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Nhungumalwa – Ngudu mpaka Magu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Nhungumalwa – Ngudu yenye urefu wa kilometa 71 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya mita 500 pamoja na *roundabout* zilijengwa katika eneo la Isandula. Aidha, mkataba wa ujenzi kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya kuanzia Magu hadi Ngudu yenye urefu wa kilomita 10 umesainiwa mwezi Mei, 2024 na kwa sasa mkandarasi yupo katika maandalizi ya kuanza ujenzi. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngw'asi Damas Kamani, swali la nyongeza.

**MHE. NGW'ASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa majimbo matatu, Jimbo la Kwimba, Jimbo la Sumve na Jimbo la Magu na ni barabara ambayo inapitisha shughuli nyingi sana za kiuchumi kwa wananchi hawa. Hizi kilomita 10 za barabara hii zilitengewa fedha katika bajeti iliyokwisha, mwaka 2023/2024, lakini mpaka sasa mkandarasi hajaweka hata vifaa *site*. Je, ni lini mkandarasi ataanza kazi rasmi katika barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuhusiana na zile kilomita 61 zilizobaki. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kilomita hizi kwa kiwango cha lami ukizingatia zimekuwa zikiahidiwa katika ilani mbalimbali za uchaguzi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ngoja kwanza, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, rudi kwenye kiti chako ukaketi Mawaziri wanasikiliza maswali. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii inaunganisha majimbo matatu, Sumve, Magu na Kwimba, tunatambua umuhimu wake na pia barabara hii iko kwenye ilani na ndiyo maana tumeanza kuijenga kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, tumeshajenga *roundabout* na sasa tumeshasaini mkataba na mkandarasi ili tuanze kujenga kwa awamu hizo kilomita 10. Mkandarasi sasa hivi yuko kwenye maandalizi ya awali kwa ajili ya kuanza hizo kilomita 10.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa sababu mpango ni kuijenga barabara hii yote, Serikali inaendelea kutafuta fedha na tukipata fedha, basi tutaijenga yote kwa pamoja, lakini kama fedha itakuwa inapatikana kwa awamu tutaendelea kuijenga kwa awamu ili kuikamilisha hiyo barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Byabato, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kutoa fedha ya ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia *roundabout* ya Rwamishenye mpaka njia panda ya Kashabo Bukoba Mjini, sasa naomba kujua ni lini ujenzi huo utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii ya njia nne inaendelea kujengwa katika Mji wa Bukoba na ilikuwa imepangwa imalizike mwaka huu. Changamoto ambayo imejitokeza ni kwamba kuna kitu kama *land slide* ambayo imeonekana, maji yanatoka chini. Kwa hiyo, sasa hivi eneo hilo tunalipitia upya ili liweze kuangaliwa kama bado barabara itaendelea kupita hapo ama tunatakiwa tuibadilishe. Baada ya kupata majibu ya wataalam, barabara hiyo itaendelea kujengwa na kukamilishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, leo ni ipi kauli ya Serikali juu ya ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba kupitia Makao Makuu ya Halmashauri ya Chitete?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, tulipokuwa kwenye Bunge la Bajeti Mwezi Juni, Mheshimiwa Waziri alilieleza Bunge kwamba, muda siyo mrefu mkandarasi atakuwa *site*, lakini hadi leo hakuna mkandarasi. Je, ni ipi kauli yako kwa Wanamomba na Wanambozi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii inaanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha ambapo utekelezaji umeanza Mwezi Julai mwaka huu. Pia, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, taratibu za kuandaa nyaraka za zabuni zinaendelea na mara zitakapokamilika tutatangaza hizo zabuni ili mkandarasi aanze kujenga Barabara hiyo ya Mlowo – Kamsamba. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Kuipandisha Hadhi Barabara ya Kutoka Mkolani Darajani – Nyakagwe Hadi Busisi**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaipandisha hadhi Barabara ya kutoka Mkolani Darajani – Nyakagwe hadi Busisi kwa kuiondoa *TARURA* na kuipeleka *TANROADS?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupandisha au kushusha hadhi barabara upo kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Sheria ya

Barabara, Na. 13 ya Mwaka 2007 na Kifungu cha 44(1) cha Kanuni za Menejimenti ya Barabara za Mwaka 2009. Kwa utaratibu huo, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe maombi ya kuipandisha hadhi barabara hiyo. Maombi hayo yatakapowasilishwa yatafanyiwa kazi na ikionekana barabara hiyo inakidhi vigezo, itapandishwa hadhi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, umuhimu wa barabara hii ambayo inapita Mwasonge – Bulale – Nyakagwe mpaka Mkolani, inaungana moja kwa moja na Daraja la Busisi na tunafahamu liko zaidi ya 90% sasa, linaelekea kukamilika. Serikali haioni umuhimu wa kutengeneza barabara hii ili kupunguza msongamano wa njia kubwa ili hii ndiyo itumike kama njia mbadala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi na bahati nzuri binafsi naifahamu hii barabara. Tumeomba wenzetu wa Mkoa wa Mwanza kupitia vikao vyao vya kisheria ambavyo tumevitaja, waweze kuleta maombi katika Wizara ya Ujenzi na wataalamu watakwenda kufanya tathmini. Kama itathibitika kwamba, ina vigezo Wizara haitasita kuipandisha hadhi hiyo barabara na sasa ianze kumilikiwa au kusimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Ujenzi wa Daraja la Kilambo**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Kilambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatafuta fedha ili iweze kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Kilambo. Baada ya kufanyiwa usanifu na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa kuwa, wenzetu wa Mozambique wameanza kutengeneza barabara ya lami karibu kilometa 20 kutoka Mozambique kuja Mto Kilambo. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali na wao wataanza kujiandaa kutengeneza barabara ya lami ambayo itatoka kwenye Kata ya Ziwani kuelekea kwenye eneo la Daraja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni eneo tunalozungumza la Daraja. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari tukaongozana na wataalamu wako wa Wizara kwenda kuona eneo ambalo ninalizungumzia mimi kwa takribani miaka mitatu mfululizo sasa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunatambua kwamba daraja hili ni muhimu. Ndiyo maana tumekuwa tukitenga kiasi kidogo cha fedha, kwa ajili ya kuweza kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, hili pia ni daraja ambalo linaunganisha nchi yetu ya Tanzania na Msumbiji kupitia Mtwara. Pia, ili Daraja hili kubwa ambalo pengine litakuwa na urefu si chini ya kilometa tatu, tuna taasisi mbalimbali ambazo ni lazima zihusike; sisi, kama Wizara ni wajenzi tu, lakini Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Nje kwa sababu, inahusisha nchi na nchi na pia, wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, wenzetu wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa sababu, ni Daraja ambalo linaunganisha nchi na nchi, tuweze kufikia maamuzi. Pia, tayari kuna mazungumzo ambayo yapo yanaendelea, yakishakamilika na sisi Wizara tukiambiwa tuanze, tutaanza kulijenga hilo daraja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda kulitembelea, niko tayari muda wowote tutakapopanga na Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, Jambo la Dharura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, jana wakati wa kipindi cha maswali mtakumbuka kulikuwa kuna hoja iliyokuwa inahusu Kituo cha Afya kilichopo Jimbo la Ilemela na nilimwomba ama nilimuagiza Mheshimiwa Mbunge alete ushahidi kwa namna Kanuni zetu zinavyotaka, lakini sikuwa nimempa tarehe ya kuleta huo Ushahidi. Sasa nimpe tarehe ya kuleta huo Ushahidi, itakuwa Tarehe 30 Mwezi Agosti, 2024. Mheshimiwa Angelina Mabula.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wako hapa Bungeni asubuhi hii na tutaanza na wageni sita ambao ni Viongozi wa Wizara ya Uchukuzi, Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege *(TAA),* Ndugu Ludovic Nduhiye - Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi; Ndugu Maseke Mabiki - Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Uchukuzi; Ndugu Biseko Chiganga - Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi - Wizara ya Uchukuzi; Ndugu Hassan Munguja - Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Sheria, Wizara ya Uchukuzi; Ndugu Musa Mbura - Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege *(TAA)* na Ndugu Pamela Mgalula, Mkurugenzi wa Sheria, Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege *(TAA),* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wengine, wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni wapiga kura wake kutoka Ilemela, Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Mwantumu Dau ambao ni wanafunzi wa Kada ya Uuguzi Ngazi ya Shahada *(Bachelor of Science in Nursing)* kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(State University of Zanzibar),* ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni mmoja wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Ndugu Joshua Onesmo Mfugale ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Mfugale kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 52 na wakufunzi wawili kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 160 na walimu 12 kutoka Shule ya Awali na Msingi, *The Glory* iliyopo Mafinga, karibuni sana wageni wetu Bungeni. Tunawashukuru kwa kuja kututembelea.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine ambalo linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba, siku ya Tarehe 31 Agosti, 2024, katika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlin, iliyopo Miyuji Jijini

Dodoma, kutafanyika Bonanza. Bonanza hili litaanza kwa maandamano yatakayoanzia Chuo cha Mipango Dodoma, Saa 12.00 asubuhi.

Bonanza litahusisha michezo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mpira wa Miguu, Bunge na *NMB*.

(ii) Mpira wa Pete, Bunge na *NMB*.

(iii) Kuvuta Kamba wanaume, Bunge na *TANESCO*.

(iv) Kuvuta Kamba wanawake, Bunge na Wizara ya Maji.

(v) Mpira wa Kikapu wanaume, Bunge na *TANAPA*.

Michezo mingine Riadha, Kutembea Mwendo wa Haraka, Kucheza Bao, Kucheza *Draft, Pool Table*, Kurusha Tufe, Kucheza Karata, Kurusha Vishale, Kukimbia na Gunia, Kufukuza Kuku, Kushindana Kupiga Danadana, Kushindana Kuruka Kamba, Kushindana Kuvaa Soksi, Kushindana Kunywa Soda na Kula Chakula kwa Haraka. Haya Mwenyekiti wa Bonanza ananiangalia hapa.

Lengo la Bonanza hili lililodhaminiwa na Benki ya *NMB PLC* ni, pamoja na kuimarisha afya, limelenga kuendeleza uhusiano wa taasisi yetu na wadau mbalimbali. Mgeni Rasmi kwenye tamasha hili anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati.

Naona na kauli mbiu imebadilika kidogo, jambo ambalo ni la msingi sana, sasa ni Shiriki Uchaguzi kwa Maendeleo ya Taifa Letu. Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kushiriki bila kukosa. Hili linatuhusu sisi sote na hatokuwepo wa kukosa.

Vilevile kama kuna Kamati ilikuwa imepewa kibali cha kusafiri kwenda kwenye mafunzo, basi vibali vyote vimefutwa kwa tangazo hili ili wote tuweze kushirikiana. Vibali hivyo vitatolewa

kwa Jumamosi ile nyingine baada ya Bunge, ili sote tuweze kushiriki kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, Hoja ya Dharura.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi.

**HOJA YA DHARURA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. Nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ya Jambo la Dharura.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya msingi ni kuhusu vitendo vinavyoendelea hapa nchini vya baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kukamata wananchi na kuwaweka ndani pasipokuwa na sababu ya msingi. Jambo hili linahatarisha haki za binadamu. Mfano, jambo hili limetokea pale jimboni kwangu, Tarehe 26 Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge kuna hoja inaletwa hapa, sasa, ili mjue kama mtaunga mkono au hamtaunga mkono ni lazima msikilize. Ndiyo maana wengine mnasimama kabla hamjasikia, halafu mnakuwa hamjui mmeunga mkono kitu gani.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, mnamo Tarehe 26 mwezi huu wa Nane, Mheshimiwa *DC* akiwa kwenye ziara yake katika Kata ya Mbingu, Kijiji cha Chiwachiwa, akienda kusikiliza mgogoro wa ardhi baina ya Msitu wa Hifadhi wa *TFS* na Wananchi wa Kijiji cha Chiwachiwa. Akiwa katika mkutano wa hadhara Diwani alileta hoja kwamba, Mheshimiwa *DC* hapa tunahitaji tu-*verify* mipaka, wananchi wanaamini bado wako kwenye eneo lao sahihi.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ilisababisha Mheshimiwa *DC* kusema, unaniharibia mkutano, kamata weka ndani. Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kijiji na baadhi ya wananchi 11 mpaka hivi sasa ninavyozungumza wako ndani.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivi vya Mheshimiwa *DC,* inasemekana wakati wa Mkutano wa Hadhara alipokea simu ya Mkuu wa Mkoa na akaiweka kwenye *loudspeaker*. Kwa hiyo, maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na *DC* wakakubaliana kuwakamata hao watu wote 11 wakiwemo watu wanne ambao ni Mheshimiwa Diwani, Mtendaji wa Kijiji, Mtendaji wa Kata na Mwenyekiti wa Kijiji.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya Mheshimiwa *DC* vimekuwa ni vya kawaida. Akienda kwenye mikutano ya hadhara anakwenda na Kamati ya Ulinzi na Usalama, wananchi hata kutoa hoja zao hawawezi, lakini cha ajabu zaidi amekuwa akikamata viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ilishawahi kutokea katika Kata ya Utengule alimkamata Mwenyekiti wa CCM wa Kata na Mwenyekiti wa Kijiji akawaweka ndani kwa siku sita, nilivyomwomba aliwatoa. Sasa kama watu wana makosa na pamoja na jitihada za Mheshimiwa Rais kuunda Tume ya Haki Jinai na Waraka Mkuu wa Haki ya Utumishi wa Umma Na.1 wa Mwaka 2023 uliotolewa tarehe 30 Oktoba, 2023, Katibu Mkuu Kiongozi alielekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, alitoa katazo kuhusu matumizi ya madaraka ya ukamataji wa watuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anafanya jitihada kubwa sana katika kusimamia misingi ya utawala bora na haki za binadamu nchini, lakini baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wa namna hii wamekuwa wakimkosea Mheshimiwa Rais, wakimchonganisha Mheshimiwa Rais na wananchi wake. Mheshimiwa Rais jambo hili likome nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, limekuwa likitokea kwa baadhi ya mikoa na siyo tu Morogoro. Naomba kutoa hoja na

Waheshimiwa Wabunge mlioko humu ndani mniunge mkono, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge bado muda wa kuunga mkono hoja. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu za Kudumu za Bunge zinatoa fursa kwa Mbunge yeyote ambaye anaona kuna jambo limetokea kwenye jamii ambalo haliwezi kufanyiwa kazi kwa utaratibu wa kawaida, kuweza kusimama kwa kutumia Kanuni ya 54 na kuliomba Bunge liache shughuli linazofanya ili liweze kujadili jambo la dharura. Sasa ili kuweza kulipa Bunge nafasi ya kujadili jambo hilo na kutoa mazingira ambayo tunaweza kuwa, kila siku kuna jambo la kujadili, basi Kanuni yetu ya 55 imeweka masharti ya jambo linaloweza kukidhi kwamba, ni la dharura.

Waheshimiwa Wabunge, jambo alilosema Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba, Mheshimiwa Kunambi, kwa maana ya kukamatwa hao watu 11 ni jambo la hivi karibuni. Hata hivyo, kwa maana ya huu utaratibu wa Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na mazingira fulani hivi Mawaziri kuwaweka watu ama kuagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuwakamata watu ni vitu ambavyo vimekuwepo. Kwa hiyo, siyo jambo jipya na kwa hivyo, siyo jambo ambalo limetokea kwa dharura kwa sababu, limekuwepo.

Kwa sababu ni jambo ambalo liko kisheria na hii Sheria imetungwa na Bunge, Sheria hii imetungwa na Bunge jamani, hata kama wewe hukuwepo humu ndani imetungwa na Bunge. Kwa hiyo, Sheria hii imetungwa na Bunge, sasa utekelezaji wake, maana yake utekelezaji wa hiki kifungu au sheria hii, ndiyo changamoto ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Mbunge.

Sasa kwa sababu, jambo hili siyo jambo jipya kwa hiyo, siwezi kuliita kwamba, ni jambo la dharura. Isipokuwa kwa changamoto aliyoisema Mbunge Serikali iko humu ndani, Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa ndani na jambo hili amelizungumza kwa kirefu kabisa, basi huyo *DC,* Mkuu wa Mkoa, hebu tufahamu kwamba, changamoto iko wapi? Kwa sababu, tukiishia kujadili hapa ndani tutatoa maelekezo gani kwa Serikali? Kwa sababu, tumetunga sheria ili iweze kufanya kazi, lakini ni kwa mazingira ambayo

itekelezwe bila kukosea haki za wale wanaohusika na itekelezwe kwa namna Bunge lilivyotaka. Kwa sababu Bunge limetoa nafasi hiyo kwa hawa Wakuu wa Mikoa na hawa Wakuu wa Wilaya kufanya hivyo pale ambapo wanaona huyu mtu ambaye wanaagiza akamatwe anahatarisha usalama wa wale watu walioko pale, ama yeye mwenyewe usalama wake unahatarishwa akiachwa uraiani.

Sasa kwa sababu Bunge halina uwezo wa kujua kwamba mazingira yaliyotolewa hiyo amri yalikuwa ni kwamba kuna hatari kwa hao waliokamatwa wanataka kupigwa pengine na wananchi ama wao wanataka kuwadhuru wananchi. Kwa hiyo kwa sababu hatuyajui mazingira tukiishia hapa kujadili na sisi tukijadili humu ndani lazima tufikie mahali ambapo tutafanya maamuzi. Sasa ili Bunge liweze kujadili hoja na kufikia mahali ambapo tunaweza kufanya maamuzi lazima Bunge liwe na taarifa hizo za ziada.

Mheshimiwa Mbunge hoja yake ni kwamba hao watu wamekamatwa na wako ndani na kwa maelezo aliyoyatoa yeye anaona utaratibu wa kisheria haujafuatwa na kwa sababu Bunge halina nafasi ya kujiridhisha na hayo mazingira basi Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa jambo hili lifanyiwe kazi Mbunge amezungumza kuhusu wananchi ambao wamekamatwa, ikiwa ziko sababu basi likishafuatiliwa Mbunge ajulishwe kwamba ziko sababu kwa nini hao watu wamekamatwa kama hayo mazingira ni yale ambayo yako kisheria.

Pungufu ya hapo kwa kweli hili alilolieleza Mheshimiwa Mbunge itabidi pengine ile sheria sasa sisi kama Bunge tuitazame upya kama inaleta changamoto kwenye utekelezaji wake. Nia ya hii sheria haikuwa mtu kuonesha nguvu aliyonayo ya kuagiza polisi kamata huyu hapana, nia yake ilikuwa ni hiyo ambayo nimeshaieleza sina haja ya kuirejea. *(Makofi)*

Kama hicho sicho kinachofanyika basi kuna haja ya kuitazama upya sheria hii ili kuondoa huo mkanganyiko wa viongozi kuanza kuogopwa sasa na wananchi maana kila wakati sasa watakuwa wanaagiza huyu akamatwe, huyu awekwe ndani

na mambo kama hayo na tumeshayaona haya yakitokea hata mtu ambaye hana mamlaka kabisa yaani kwenye sheria hajatajwa na yeye anasema kamata weka ndani, sasa hii haiwezekani, haiwezekani!

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu hili naomba ulifuatilie halafu Mbunge ajulishwe ni nini kinaendelea huko kwenye jimbo lake kwa sababu wananchi kuwekwa ndani kwa kusema tu hoja hadharani haipendezi wala si jambo ambalo sheria ilikusudia kulifikia hivyo lakini kama kuna jambo lingine la ziada lililofanyika basi Mheshimiwa Waziri Mkuu ukishalipata mjulishe Mbunge ili yeye awe na utulivu lakini pia aweze kuwajulisha wananchi anaowawakilisha kwamba wale wenzetu ambao wako kule ndani sababu ni hizi, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kulisema hilo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada unakuja kusomwa kwa mara ya pili na sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Mkutano wa Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia Watanzania. Aidha, tunaendelea pia kumshukuru Mwenyezi

Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu kuendelea kutunza Tunu za Taifa letu ikiwemo amani, utulivu na upendo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa jinsi mnavyoendelea kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, kwa namna ya kipekee niwashukuru Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa majadiliano yote yaliyofanyika ndani ya Kamati na kwa wadau mbalimbali kuhusu Muswada huu muhimu wa utungaji wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024. Hakika Kamati hii imetimiza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutumia nafasi kumpongeza Mheshimiwa Hamza Johari aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunakupongeza sana na tunakutakia utekelezaji mwema wa majukumu yako mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024. Lengo la kutungwa kwa sheria hii ni kuweka mfumo madhubuti na thabiti wa kisheria wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Muswada unakusudia kutatua changamoto mbalimbali za usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege ambazo

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekuwa ikikumbana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Sita. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa, utaratibu wa kuanza kutumika kwa Sheria inayotungwa, matumizi yake pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika masharti mbalimbali yanayopendekezwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania. Sehemu hii pia inaainisha majukumu na mamlaka ya *TAA*, uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi, mamlaka ya Bodi, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na masuala mengine yanayohusu maafisa na watumishi wa Mamlaka. Kwa mujibu wa masharti ya Muswada, Mamlaka inayopendekezwa kuanzishwa itaendelea kutekeleza majukumu yake kama Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti kuhusu usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege. Katika sehemu hii, Mamlaka inapendekezwa kupewa jukumu la kuanzisha rejista ya taarifa za viwanja vya ndege na kuanzisha Kamati mbalimbali katika kila kiwanja cha ndege kwa lengo la kutekeleza na kuwezesha shughuli za viwanja vya ndege. Aidha, sehemu hii inaweka masharti yanayoiwezesha Mamlaka kuweka ada na tozo za huduma mbalimbali za viwanja vya ndege, mamlaka ya kufuatilia maeneo ya vizuizi vya viwanja vya ndege kwa kufanya ufuatiliaji na ukaguzi kwenye maeneo ambayo yako karibu na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, sehemu hii inaainisha masuala yanayohusu ubora wa huduma zinazotolewa katika viwanja vya ndege, usalama katika viwanja vya ndege, usimamizi wa maegesho ya ndege, uondoaji wa ndege, vyombo vya usafiri na vifaa vilivyoharibika kwenye eneo la kuruka ndege, utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi, dharura kwenye viwanja vya ndege, uchaguzi wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege,

mipango, usanifu na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Serikali, matengenezo ya viwanja vya ndege pamoja na usimamizi wa ardhi, miundombinu na mali katika viwanja vya ndege vya Serikali. Masharti yanayopendekezwa katika sehemu hii yanalenga kuhakikisha viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali vinasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango vya udhibiti vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inaweka masharti ya fedha. Masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya fedha vya Mamlaka na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu za Mamlaka. Vyanzo hivyo ni pamoja na fedha zitakazotengwa na Bunge na ada na tozo zitakazotozwa katika huduma mbalimbali katika viwanja vya ndege. Sehemu hii inaainisha pia masharti kuhusu uwekezaji wa fedha za Mamlaka, utaratibu wa uidhinishaji wa bajeti ya Mamlaka na uwasilishaji wa taarifa ya mwaka ya shughuli za Mamlaka. Masharti ya sehemu hii yanalenga kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha ya Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inaweka masharti kuhusu makosa na adhabu. Katika sehemu hii, Muswada unaainisha makosa mbalimbali na adhabu kwa mtu atakayetenda makosa hayo. Makosa hayo ni pamoja na kumiliki vitu hatarishi kama vile bunduki na vilipuzi katika maeneo yanayodhibitiwa au yanayokatazwa, kutenda vitendo vinavyoweza kuhatarisha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege, kufanya uharibifu wa miundombinu ya viwanja vya ndege, kumzuia au kumkwamisha mtumishi wa Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake chini ya sheria inayopendekezwa na kuzuia au kuingilia matumizi sahihi ya viwanja vya ndege. Lengo la masharti haya ni kuhakikisha uzingatiaji wa masharti mbalimbali ya sheria inayopendekezwa yanazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inaweka masharti ya jumla yakiwemo: Mamlaka ya Waziri kutoa maelekezo kwa Mamlaka; Utekelezaji wa miongozo inayotolewa na Mdhibiti; Kinga ya maafisa na watumishi wa Mamlaka dhidi ya uwajibikaji binafsi; na Mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na kufutwa

kwa Sheria ya Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Viwanja vya Ndege ya mwaka 1974.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; nihitimishe kwa kukushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Muswada huu na nichukue nafasi hii kuliomba Bunge la Tukufu kujadili Muswada huu wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024 na kuridhia Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye upitishwe kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA AWALI YA MHE. MAKAME MNYAA. MBARAWA (MB), WAZIRI WA UCHUKUZI KWA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA WA MWAKA 2024 KATIKA MKUTANO WA KUMI NA SITA KIKAO CHA PILI TAREHE 28 AGOSTI, 2024 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Mkutano wa Bunge lako tukufu kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia Watanzania. Aidha, tunaendelea pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu kuendelea kutunza tunu za Taifa letu ikiwemo amani, utulivu na upendo.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Naibu Spika kwa jinsi mnavyoendelea kuliongoza Bunge hili, hususan katika vipindi vya kujadili masuala makubwa na muhimu kwa nchi yetu. Aidha, kwa namna ya kipekee niwashukuru Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa majadiliano yote yaliyofanyika ndani ya kamati na kwa wadau mbalimbali kuhusu muswada huu muhimu wa utungaji wa Sheria ya

Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024. Hakika Kamati hii imetimiza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu kwa umahiri mkubwa.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, napenda kutumia nafasi kumpongeza **Mheshimiwa Hamza Johari** aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*Tanzania Civil Aviation Aurthority*-TAA) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunakupongeza Sana na tunakutakia utekelezaji mwema wa majukumu yako mapya.

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024.

**B. UWASILISHAJI WA MUSWADA**

6. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024. Lengo la kutungwa kwa Sheria hii ni kuweka mfumo madhubuti na thabiti wa kisheria wa Usimamizi, Uendeshaji na Uendelezaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Muswada unakusudia kutatua changamoto mbalimbali za usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege ambazo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekuwa ikikumbana nazo katika utekelezaji wa makujukumu yake.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Sita. Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la Sheria inayopendekezwa, utaratibu wa kuanza kutumika kwa Sheria inayotungwa, matumizi yake pamoja na tafsiri za misamiati

mbalimbali iliyotumika katika masharti mbalimbali yanayopendekezwa katika Muswada.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA). Sehemu hii pia inaainisha majukumu na mamlaka ya TAA, uanzishwaji wa Bodi ya Wakurugenzi, mamlaka ya Bodi, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na masuala mengine yanayohusu maafisa na watumishi wa Mamlaka. Kwa mujibu wa masharti ya Muswada, Mamlaka inayopendekezwa kuanzishwa itaendelea kutekeleza majukumu yake kama Mamlaka.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tatu ya Muswada inaweka masharti kuhusu usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege. Katika Sehemu hii, Mamlaka inapendekezwa kupewa jukumu la kuanzisha rejista ya taarifa za viwanja vya ndege na kuanzisha kamati mbalimbali katika kila kiwanja cha ndege kwa lengo la kutekeleza na kuwezesha shughuli za viwanja vya ndege. Aidha, Sehemu hii inaweka masharti yanayoiwezesha Mamlaka kuweka ada na tozo za huduma mbalimbali za viwanja vya ndege, mamlaka ya kufuatilia maeneo ya vizuizi vya viwanja vya ndege kwa kufanya ufuatiliaji na ukaguzi kwenye maeneo ambayo yako karibu na viwanja vya ndege. Kadhalika, Sehemu hii inaainisha masuala yanayohusu ubora wa huduma zinazotolewa katika viwanja vya ndege, usalama katika viwanja vya ndege, usimamizi wa maegesho ya ndege, uondoaji wa ndege, vyombo vya usafiri na vifaa vilivyoharibika kwenye eneo la kuruka ndege, utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi, dharura kwenye viwanja vya ndege, uchaguzi wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege, mipango, usanifu na ujenzi wa viwanja vya ndege, matengenezo ya viwanja vya ndege pamoja na usimamizi wa ardhi, miundombinu na mali katika viwanja vya ndege. Masharti yanayopendekezwa katika Sehemu hii yanalenga kuhakikisha viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali vinasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango vya udhibiti vilivyowekwa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Nne ya Muswada inaweka masharti ya fedha. Masharti hayo ni pamoja na vyanzo vya fedha vya Mamlaka na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu za Mamlaka. Vyanzo hivyo ni pamoja na fedha zitakazotengwa na Bunge na ada na tozo zitakazotozwa katika huduma mbalimbali katika viwanja vya ndege. Sehemu hii inaainisha pia masharti kuhusu uwekezaji wa fedha za Mamlaka, utaratibu wa uidhinishaji wa bajeti ya Mamlaka na uwasilishaji wa taarifa ya mwaka ya shughuli za Mamlaka. Masharti ya Sehemu hii yanalenga kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha ya Mamlaka.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Tano ya Muswada inaweka masharti kuhusu makosa na adhabu. Katika Sehemu hii, Muswada unaainisha makosa mbalimbali na adhabu kwa mtu atakayetenda makosa hayo. Makosa hayo ni pamoja na kumiliki vitu hatarishi kama vile bunduki na vilipuzi katika maeneo yanayodhibitiwa au yaliyokatazwa, kutenda vitendo vinavyoweza kuhatarisha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege, kufanya uharibifu wa miundombinu ya kiwanja cha ndege, kumzuia au kumkwamisha mtumishi wa Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria inayopendekezwa na kuzuia au kuingilia matumizi sahihi ya viwanja vya ndege. Lengo la masharti haya ni kuhakikisha uzingatiaji wa masharti mbalimbali ya Sheria inayopendekezwa.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sehemu ya Sita ya Muswada inaweka masharti ya jumla yakiwemo mamlaka ya Waziri kutoa maelekezo kwa Mamlaka, utekelezaji wa miongozo inayotolewa na Mdhibiti, kinga ya maafisa na watumishi wa Mamlaka dhidi ya uwajibikaji binafsi, mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na kufutwa kwa Sheria ya Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Viwanja vya Ndege ya mwaka 1974.

## C: HITIMISHO

**13.** ***Mheshimiwa Spika**,* nihitimishe kwa kukushukuru tena kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Muswada huu na nichukue nafasi

hii kuomba Bunge la Tukufu kujadili Muswada huu wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania Mwaka 2024 na kuridhia Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye upitishwe kuwa Sehemu ya Sheria za Nchi.

14. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Machi, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 28 Juni, 2024, katika Kikao cha Hamsini na Sita cha Mkutano wa Kumi na Tano. Baada ya hatua hiyo na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni 136(14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ili Kamati iujadili na kuufanyia uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa

mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteKEleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada, ambayo yaliwasilishwa na Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa siku ya Jumanne, tarehe 13 Agosti, 2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2), Kamati ilipanga kufanya Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* siku ya Jumatano tarehe 14 Agosti, 2024, ambapo Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau yaliyowasilishwa. Maoni yaliyowasilishwa na kujadiliwa na Kamati yaliandaliwa na Chama cha Wadau wa Usafiri wa Anga Tanzania *(Tanzania Aviation Operators' Association)*.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati kabisa, wadau waliowasilisha maoni yao, ambayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya Mwaka 2024 na unalenga kuweka mfumo wa kisheria wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Serikali. Aidha, Muswada unakusudia kutatua changamoto mbalimbali za usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege ambazo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekuwa ikikumbana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake, kama ilivyokuwa katika uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA)* chini ya Kampuni ya *KADCO*.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mambo ambayo Kamati imebaini ni kwamba, pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 404 la mwaka 1999, Mamlaka iliyopo sasa imekuwa ikitekeleza majukumu yake kama Wakala chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245 na kusimamiwa na Bodi ya Ushauri ambayo ina mamlaka finyu. Aidha, baadhi ya viwanja vya ndege vya

Serikali viliendelea kusimamiwa na kuendeshwa na taasisi nyingine za Serikali hali ambayo ilisababisha kutowekupo kwa mfanano katika usimamizi na uendeshaji wa jumla wa viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Sheria inayopendekezwa kutungwa na Muswada huu inapendekeza kuipatia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA),* mamlaka kamili ya kisheria ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi chini ya Bodi ya Utendaji ambayo mwenyekiti wake atateuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ilifanya uchambuzi wa kina wa ibara mbalimbali za Muswada. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yalijadiliwa kwa kina ili kuboresha maudhui yake. Moja kati ya eneo lililojadiliwa na Kamati kupendekeza maboresho ya Jina refu la Muswada ambapo Kamati ilishauri Serikali kuongeza neno 'uanzishaji' ili jina hilo lisomeke kama ifuatavyo: "Sheria ya Kuweka Masharti Madhubuti ya Uanzishaji, Uendelezaji, Usimamizi, Uendeshaji na Utunzaji wa Viwanja Vya Ndege; Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu ya Mamlaka yake na masuala mengine yanayohusiana na hayo."

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa, maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali umezingatiwa katika kuboresha maudhui ya Muswada huu. Hata hivyo, kwa ajili ya kuweka Kumbukumbu za Bunge sawa, nitazungumzia kwa msisitizo baadhi ya sehemu na ibara za Muswada ambazo Kamati ilizifanyia uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inajumuisha jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika, mipaka ya matumizi, pamoja na kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya tatu ambayo inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali, Kamati ilifanya tathmini ya maneno

"kitendo cha uvamizi kinyume cha sheria" na kubaini kwamba tafsiri iliyopo ilikuwa haijitoshelezi kwa kutobainisha uwezo wa kitendo hicho kujumuisha kupanga au kushiriki kama ambavyo Muswada unavyosomeka. Hivyo basi, Kamati iliishauri Serikali kuboresha tafsiri hiyo kwa kujumuisha maneno hayo ili kuongeza wigo wa kosa la uvamizi kinyume cha sheria katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada, Ibara ya 21 inaipa Mamlaka wajibu wa kuhakikisha kunakuwepo na usalama katika viwanja vya ndege ikiwemo upatikanaji wa huduma za zimamoto na uokoaji, udhibiti wa wanyama na ndege. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitathmini hali halisi ya uratibu wa huduma za zimamoto na uokoaji ili kuona iwapo masharti yaliyomo katika Muswada, yataongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, bila kuathiri masharti ya sheria nyingine za nchi, Kamati ina mashaka iwapo kwa masharti yaliyopo katika Muswada kwa namna Ibara ya 21 ilivyoandikwa, kuna uwezekano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kutokuwa na mamlaka kamili ya kiusimamizi na kiuratibu hasa kwa kuzingatia upekee wa huduma za zimamoto na uokoaji katika viwanja vya ndege ambavyo inahitaji ujuzi wa ziada kwa kuzingatia mifumo na viwango vya kimataifa. Aidha, kwa kuliweka jambo hilo chini ya uratibu wa taasisi moja kutaongeza uwajibikaji endapo kutatokea janga litakalohitaji huduma ya zimamoto na uokoaji katika Viwanja vya Ndege vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inahusu masharti ya fedha. Ibara ya 32 ya Muswada inaainisha vyanzo vya fedha za Mamlaka ambapo Kamati imebaini kwamba, katika vyanzo vya fedha vilivyoorodheshwa, Muswada haujaweka bayana iwapo Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Service Charge)* ni moja ya vyanzo vya fedha za Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti wa tathmini iliyofanywa, Kamati imebaini kwamba, mwaka 1962 Serikali ilitunga Sheria ya *Airport Service Charge Act* Sura ya 365 kwa ajili ya ukusanyaji wa

Tozo ya Huduma kwa Abiria katika viwanja vya ndege. Sheria hiyo kupitia Kifungu cha 3(1) ilianzisha Tozo ya Huduma kwa Abiria ambayo hutozwa kwa kila abiria anayetumia kiwanja cha ndege kwa ajili ya kuanza safari.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hiyo, mawakala wa ukusanyaji wa tozo hiyo ni mashirika ya ndege na mawakala wa usafiri wa ndege ambao huikusanya na kuiwasilisha kwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Sheria hii inasimamiwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati imebaini kwamba katika vipindi tofauti, Wizara iliyokuwa na dhamana ya masuala ya uchukuzi iliwasilisha mapendekezo ya kupatiwa Tozo ya Huduma kwa Abiria ili kuweza kumudu gharama za uendeshaji na ukarabati wa miundombinu katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge la Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2005/2006, aliyekuwa Waziri mwenye dhamana wa Fedha alielekeza kuwa makusanyo yote yatokanayo na Tozo ya Huduma kwa Abiria yaelekezwe *TAA*. Kufuatia maelekezo hayo, Wizara ya Fedha ilikuwa ikiipatia *TAA* fedha zitokanazo na tozo ya huduma abiria kwa mfumo wa *retention*. Hata hivyo, mnamo mwaka 2017, Serikali ilifuta utaratibu wa *retention* kwa Taasisi za Umma kupitia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kifungu Na. 58 (a-c).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba kutorejeshwa kwa fedha za makusanyo yanayotokana na Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Service Charge)* ambacho ni chanzo kikubwa cha mapato katika viwanja vya ndege nchini, kunasababisha ufinyu wa mapato ya Taasisi na hivyo kusababisha *TAA* kushindwa kusimika, kukarabati na kuboresha miundombinu, mifumo, mitambo na vifaa katika viwanja vya ndege hali inayopelekea huduma duni kwa abiria wanaotumia viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano ya chanzo hicho cha mapato wakati wa uchambuzi wa Muswada, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho ya msingi katika sheria nyingine za

nchi ili kuiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwa na uhuru kamili wa kukusanya na kutumia Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Service Charge)* kwa kuzingatia miongozo thabiti ya matumizi bora ya fedha za umma na ili kuboresha utendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini.

Mheshimiwa Spika, ushauri ulitolewa kwa kuzingatia ukweli kwamba, Kamati hairidhishwi na masuala yafuatayo:-

(1) Hali duni ya miundombinu ya jengo la kwanza la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na majengo ya abiria katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Dodoma, Mtwara, Mafia, Lindi na Nachingwea ambavyo ni chakavu na hupelekea abiria kutoridhishwa na huduma wanapopita katika majengo haya;

(2) *TAA* kushindwa kusimika mifumo na mitambo ya kisasa ya TEHAMA katika viwanja vya ndege. Mifumo hii inaposimikwa, hurahisisha uchakataji wa abiria na mizigo pamoja na kupunguza muda na gharama za kumhudumia abiria; na

(3) *TAA* kushindwa kuendana na uboreshaji wa masuala kiusalama hasa kwenye utekelezaji wa viwango vinavyotolewa na *ICAO* juu ya masuala hayo. Kwa mfano *TAA* inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa mitambo ya kuzima moto ambapo kwa sasa ilitakiwa kuwa na jumla ya mitambo 65 katika viwanja vya ndege vinavyofanya kazi, lakini kiuhalisia *TAA* ina mitambo 28 tu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa maelekezo kwamba imepokea na kuzingatia maoni ya Kamati. Aidha, Serikali iliitaarifu Kamati kwamba mchakato wa majadiliano kuhusu mapendekezo hayo unaendelea ndani ya Serikali na kwamba itahakikisha suala hilo linakamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sehemu ya Tano ya Muswada, sehemu hii inahusu makosa na adhabu. Mathalani, Ibara ya 40 inazungumzia makosa na adhabu za udanganyifu. Kamati imebaini kwamba Ibara hiyo haikuweka ukomo wa chini wa

adhabu ya kifungo. Kwa kutoweka ukomo wa chini wa adhabu ya kifungo, masharti ya Ibara hiyo yanaweza kutumika vibaya kwa kutoa adhabu ambayo haiendani na kosa, mfano kifungo cha siku moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina na Serikali, Kamati ilishauri kwamba Ibara hiyo ifanyiwe marekebisho ya msingi ili kuondoa uwezekano wa sheria inayopendekezwa kuweka mwanya wa matumizi mabaya katika kutoa adhabu ya kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu kuhusu Maoni na Ushauri wa Kamati; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwasilisha Muswada wa Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka wa 2024 ambao una madhumuni ya kuanzisha, kuendeleza, kusimamia, kuendesha na kutunza viwanja vya ndege nchini. Sheria inayopendekezwa, pia itaanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na kuainisha majukumu ya mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayopendekezwa, iwapo itasimamia vizuri, itaiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuongeza ufanisi wake na hatimaye kuongeza ubora wa huduma zitolewazo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Kwa muktadha huo, na kwa kuzingatia ukweli kwamba viwanja vya ndege ni lango la kiuchumi, kiutalii na kimaendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba viwanja vya ndege vya Serikali nchini vinakidhi vigezo vya *ICAO* katika ubora wa miundombinu na huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika maoni na ushauri mahsusi, kuhusu vyanzo vya mapato vya mamlaka; katika Mkutano wa Bunge uliopita wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati iliishauri Serikali ipasavyo kuhusu umuhimu wa kubakiza fedha zitokanazo na Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Retention of Passengers' Service Charge)* kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kuwasilisha marekebisho ya sheria yatakayoweka utaratibu wa kubakiza kwa

*TAA* fedha zitokanazo na tozo hiyo ili kuipunguzia taasisi hiyo utegemezi wake kwa Serikali Kuu na kuiwezesha kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Aidha, Kamati ya Bajeti iliitaka Serikali kuwasilisha fedha zote zinazokusanywa na zitakazokusanywa katika mwaka wa fedha 2024/2025 kutoka kwenye chanzo hiki kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi wa Kamati katika Muswada ambao umebaini kwamba sheria inayopendekezwa kutungwa sasa haina masharti mahsusi ambayo yataiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* kukusanya na kubakiza Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Services Charge)*, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(1) Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa pamoja zifanye upembuzi yakinifu kuhusu utaratibu bora wa kukusanya, kubakiza na kutumia Tozo ya Huduma kwa Abiria kwa asilimia 100 kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania; na

(2) Kuweka masharti ya kisheria ambayo sasa yataiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kutumia mapato yatokanayo na tozo hiyo kwa uhuru na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama wa abiria na watumiaji wa viwanja wa ndege, Kamati inatambua na kuthamini jitihada za Serikali katika kusimamia usalama wa abiria na watumiaji wa viwanja vya ndege nchini. Pamoja na hayo, Kamati ina maoni kwamba uratibu wa masuala ya usalama hususan katika kukabiliana na hatari zitokanazo na majanga ya moto katika viwanja vyetu, unapaswa kuwekwa utaratibu maalum ambao utaiwezesha Mamlaka kutoa huduma hiyo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(1) Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka nyingine yeyote husika, kufanya

upembuzi wa kina ili kubaini namna bora za kisheria ambazo zitawezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuwa na Kikosi cha Kukabiliana na Moto na Uokoaji *(Airports Firefighting Brigade and Rescue Service)* ili kuongeza weledi utakaokidhi viwango vya Kimataifa; na

(2) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuandaa mapendekezo ya kuanzisha Kikosi cha Kukabiliana na Moto na Uokoaji *(Airports Firefighting Brigade and Rescue Service)* na namna ambavyo kitajumuishwa katika Muundo wa Mamlaka kwa namna ambayo itawezesha kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ni hitimisho. Nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao katika kutekeleza majukumu yao Kikatiba, walichambua, kujadili na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge, akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge, kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati kwa uchambuzi wa Muswada. Vilevile, nawashukuru Watendaji wa Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha Uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mbunge. Kwa kuzingatia kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameteuliwa hivi karibuni na kwamba yeye ni mdau wa muda mrefu wa sekta ya anga nchini inayosimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, nitumie fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kumpongeza kwa kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kushika nafasi hiyo muhimu. Tunamtakia heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA YA MWAKA 2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Machi, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya Mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza tarehe 28 Juni, 2024 katika Kikao cha Hamsini na Sita cha Mkutano wa Kumi na Tano. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na

**Kanuni 136 (14)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ili Kamati iujadili na kuufanyia uchambuzi.

### 1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa **Kifungu cha 7(1) (b)** cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, kama ilivyo desturi, Kamati ilianza uchambuzi wake kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada, ambayo yaliwasilishwa na Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) siku ya Jumanne tarehe 13 Agosti, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya hatua hiyo, kwa mujibu wa **Kanuni ya 97 (2)**, Kamati ilipanga kufanya Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau *(Public Hearing)* siku ya Jumatano tarehe 14 Agosti, 2024 ambapo Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau yaliyowasilishwa. Maoni yaliyowasilishwa na kujadiliwa na Kamati yaliandaliwa na Chama cha Wadau wa Usafiri wa Anga Tanzania *(Tanzania Aviation Operators' Association)*.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati kabisa, wadau waliowasilisha maoni yao, ambayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024 ulifanyiwa uchambuzi na Kamati kwa kuhakiki na kufanya upembuzi wa maudhui, masharti, mpangilio, na dhamira kwa ujumla. Katika uchambuzi huo, Kamati ilijielekeza

katika mambo muhimu ya jumla pamoja na masharti mahsusi yanayopatikana katika Ibara mbalimbali za Muswada.

Aidha, Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine katika suala uendeshaji na usimamizi wa viwanja vya ndege na kufanya uchanganuzi linganifu *(comparative analysis)* kwa lengo la kuboresha masharti yanayopendekezwa na Muswada.

### 2.2 Upembuzi wa Maudhui

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya Mwaka 2024 na unalenga kuweka mfumo wa kisheria wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Serikali. Aidha, Muswada unakusudia kutatua changamoto mbalimbali za usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege ambazo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekuwa ikikumbana nazo katika utekelezaji wa makujukumu yake, kama ilivyokuwa katika uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) chini ya Kampuni ya KADCO.

**Mheshimiwa Spika,** moja kati ya mambo ambayo Kamati imebaini ni kwamba, pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 404 la mwaka 1999 Mamlaka iliyopo sasa imekuwa ikitekeleza majukumu yake kama Wakala chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245, na kusimamiwa na Bodi ya Ushauri ambayo ina mamlaka finyu. Aidha, baadhi ya viwanja vya ndege vya Serikali viliendelea kusimamiwa na kuendeshwa na taasisi nyingine za Serikali hali ambayo ilisababisha kutowekupo kwa mfanano katika usimamizi na uendeshaji wa jumla wa viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, Sheria inayopendekezwa kutungwa na Muswada huu inapendekeza kuipatia Mamlaka ya Viwanja Ndege (TAA) mamlaka kamili kisheria ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi chini ya Bodi ya Utendaji ambayo Mwenyekiti wake atateuliwa na Rais.

### 2.3 Uchambuzi Kuhusu Masharti ya Ibara Mbalimbali za Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ilifanya uchambuzi wa kina wa Ibara mbalimbali za Muswada. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yalijadiliwa kwa kina ili kuboresha maudhui yake. Moja kati ya eneo lililojadiliwa na Kamati kupendekeza maboresho, ni Jina Refu la Muswada ambapo Kamati ilishauri Serikali kuongeza neno "uanzishaji" ili jina hilo lisomeke kama ifuatavyo: -

"*Sheria ya kuweka masharti madhubuti ya **uanzishaji**, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege; kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na kuainisha majukumu na mamlaka yake, na masuala mengine yanayohusiana na hayo.*"

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa, maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali umezingatiwa katika kuboresha maudhui ya Muswada huu. Hata hivyo, kwa ajili ya kuweka Kumbukumbu za Bunge sawa, nitazungumia kwa msisitizo baadhi ya sehemu na ibara za muswada ambazo Kamati ilizifanyia uchambuzi.

#### 2.3.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inajumuisha Jina la Sheria, Tarehe ya Kuanza Kutumika, Mipaka ya Matumizi, pamoja na kutoa Tafsiri ya Maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, katika **Ibara ya 3** ambayo inatoa tafsiri ya maneno mbalimbali, Kamati ilifanya tathimini ya maneno "**kitendo cha uvamizi kinyume cha sheria**", na kubaini kwamba tafsiri iliyopo ilikuwa haijitoshelezi kwa kutobainisha uwezo wa kitendo hicho kujumuisha kupanga au kushiriki kama ambavyo Muswada unasomeka. Hivyo basi, Kamati iliishauri Serikali kuboresha tafsiri hiyo kwa kujumuisha maneno hayo ili kuongeza

wigo wa kosa la uvamizi kinyume cha sheria katika maeneo yasiyoruhusiwa.

### 2.3.2 Sehemu ya Tatu ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, **Ibara ya 21** inaipa Mamlaka wajibu wa kuhakikisha kunakuwepo na usalama katika viwanja vya ndege ikiwemo upatikanaji wa huduma za zimamoto na uokoaji, udhibiti wa Wanyama na ndege. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitathmini hali halisi ya uratibu wa huduma za zimamoto na uokoaji, ili kuona iwapo masharti yaliyomo katika Muswada, yataongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma hizo.

**Mheshimiwa Spika,** bila kuathiri masharti ya sheria nyingine za nchi, Kamati ina mashaka iwapo kwa masharti yaliyopo katika Muswada kwa namna Ibara ya 21 ilivyoandikwa, kuna uwezekano wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kutokuwa na mamlaka kamili ya kiusimamizi na kiuratibu, hasa kwa kuzingatia upekee wa huduma za zimamoto na uokoaji katika viwanja vya ndege, ambayo inahitaji ujuzi wa ziada kwa kuzingatia mifumo na viwango vya kimataifa. Aidha, kwa kuliweka jambo hilo chini ya uratibu wa taasisi moja, kutaongeza uwajibikaji endapo kutatokea janga litakalohitaji huduma ya zimamoto na uokoaji katika Viwanja vya Ndege vya Serikali.

### 2.3.3 Sehemu ya Nne ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu Masharti ya Fedha. **Ibara ya 32** ya Muswada inaainisha Vyanzo vya Fedha za Mamlaka ambapo Kamati imebaini kwamba, katika vyanzo vya fedha vilivyoorodheshwa, Muswada haujaweka bayana iwapo Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Service Charge)* ni moja ya vyanzo vya fedha za Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika**, katika utafiti na tathmini iliyofanywa, Kamati imebaini kwamba, Mwaka 1962 Serikali ilitunga Sheria ya '*Airport Service Charge Act' Sura ya 365* kwa ajili ya ukusanyaji wa Tozo ya huduma kwa abiria katika viwanja vya ndege. Sheria hiyo kupitia Kifungu cha 3(1) ilianzisha Tozo ya Huduma kwa Abiria

ambayo hutozwa kwa kila abiria anayetumia kiwanja cha ndege kwa ajili ya kuanza safari. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, mawakala wa ukusanyaji wa tozo hiyo ni mashirika ya ndege na mawakala wa usafiri wa ndege ambao huikusanya na kuiwasilisha kwa Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Sheria hii inasimamiwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia kwamba, katika vipindi tofauti, Wizara iliyokuwa na dhamana na masuala ya uchukuzi iliwasilisha mapendekezo ya kupatiwa Tozo ya Huduma kwa Abiria ili kuweza kumudu gharama za uendeshaji na ukarabati wa miundombinu katika viwanja vya ndege.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia katika Bunge la Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006, aliyekuwa Waziri mwenye dhamana wa Fedha alielekeza kuwa makusanyo yote yatokanayo na Tozo ya huduma kwa abiria yaelekezwe TAA. Kufuatia maelekezo hayo, Wizara ya Fedha ilikuwa ikiipatia TAA fedha zitokanazo na tozo ya huduma abiria kwa mfumo wa *'retention'*. Hata hivyo mnamo mwaka 2017, Serikali ilifuta utaratibu wa *'retention'* kwa Taasisi za Umma kupitia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 Kifungu Na. 58 (a-c).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, kutorejeshwa kwa fedha za makusanyo yanayotokana na Tozo ya Huduma kwa Abiria (PSC), ambacho ni chanzo kikubwa cha mapato katika viwanja vya ndege nchini, kunapelekea ufinyu wa mapato ya Taasisi na hivyo kusababisha TAA kushindwa kusimika, kukarabati na kuboresha miundombinu, mifumo, mitambo na vifaa katika viwanja vya ndege hali inayopelekea huduma duni kwa abiria wanaotumia viwanja vyetu.

**Mheshimiwa Spika**, Katika majadiliano ya chanzo hicho cha mapato wakati wa uchambuzi wa Muswada, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho ya msingi katika Sheria nyingine za nchi ili kuiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwa na uhuru kamili wa kukusanya na kutumia Tozo ya Huduma kwa Abiria (PSC) kwa kuzingatia miongozo thabiti ya matumizi bora ya

fedha za umma na ili kuboresha utendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini. Ushauri ulitolewa kwa kuzingatia ukweli kwamba, Kamati hairidhishwi na masuala yafuatayo: -

a) Hali duni ya miundombinu ya jengo la kwanza la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; na majengo ya abiria katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Dodoma, Mtwara, Mafia, Lindi na Nachingwea ambavyo ni chakavu na hupelekea abiria kutoridhishwa na huduma wanapopita katika majengo haya;

b) TAA kushindwa kusimika mifumo na mitambo ya kisasa ya TEHAMA katika viwanja vya ndege. Mifumo hii inaposimikwa, hurahisisha uchakataji wa abiria na mizigo pamoja na kupunguza muda na gharama za kumhudumia abiria; na

c) TAA kushindwa kuendana na uboreshaji wa masuala kiusalama hasa kwenye utekelezaji wa viwango vinavyotolewa na ICAO juu ya masuala hayo. Kwa mfano TAA inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa mitambo ya kuzima moto ambapo kwa sasa ilitakiwa kuwa na jumla ya mitambo 65 katika viwanja vya ndege vinavyofanya kazi lakini kiuhalisia TAA ina mitambo 28 tu.[1]

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa maelezo kwamba imepokea na kuzingatia maoni ya Kamati. Aidha Serikali iliitaarifu Kamati kwamba, mchakato wa majadiliano kuhusu mapendekezo hayo unaendelea ndani ya Serikali na kwamba itahakikisha suala hilo linakamilika mapema iwezekanavyo.[2]

### 2.3.4 Sehemu ya Tano ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu Makosa na Adhabu. Mathalani, Ibara ya 40 inazungumzia makosa na adhabu za udanganyifu. Kamati imebaini kwamba, Ibara hiyo haikuweka ukomo wa chini wa adhabu ya kifungo. Kwa kutoweka ukomo wa chini wa adhabu ya kifungo, masharti ya Ibara hiyo yanaweza

[1] Majadiliano ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu

[2] Majibu ya Serikali Kuhusu Maoni ya Kamati Katika Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania 2024

kutumika vibaya kwa kutoa adhabu ambayo haiendani na kosa. Mf. Kifungo cha siku moja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano ya kina na Serikali, Kamati ilishauri kwamba Ibara hiyo ifanyiwe marekebisho ya msingi ili kuondoa uwezekano wa Sheria inayopendekezwa kuweka mwanya wa matumizi mabaya katika kutoa adhabu ya kosa hilo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwasilisha Muswada wa Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka wa 2024 ambao una madhumuni ya kuanzisha, kuendeleza, kusimamia, kuendesha na kutunza viwanja vya ndege nchini. Sheria inayopendekezwa, pia itaanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na kuainisha majukumu na mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria inayopendekezwa, iwapo itasimamia vizuri, itaiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuongeza ufanisi wake na hatimaye kuongeza ubora wa huduma zitolewazo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Kwa muktadha huo, na kwa kuzingatia ukweli kwamba viwanja vya ndege ni lango la kiuchumi, kiutalii na kimaendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, Viwanja vya Ndege vya Serikali nchini vinakidhi vigezo vya ICAO katika ubora wa miundombinu, huduma za msingi.

### 3.2 Maoni na Ushauri Mahsusi

#### 3.2.1 Vyanzo vya Mapato vya Mamlaka

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Bunge uliopita wakati wa Mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati iliishauri Serikali ipasavyo kuhusu umuhimu wa

kubakiza fedha zitokanazo na tozo ya huduma kwa abiria (retention of passengers' service charge) kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Kamati ilishauri Serikali kuwasilisha marekebisho ya sheria yatakayoweka utaratibu wa kubakiza kwa TAA fedha zitokanazo na tozo hiyo ili kuipunguzia taasisi hiyo utegemezi wake kwa Serikali Kuu na kuiwezesha kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Aidha, Kamati ya Bajeti iliitaka Serikali kuwasilisha fedha zote zinazokusanywa na zitakazokusanywa katika mwaka wa fedha 2024/2025 kutoka kwenye chanzo hiki kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Uchambuzi wa Kamati katika Muswada ambao umebaini kwamba, Sheria inayopendekezwa kutungwa sasa haina masharti mahsusi ambayo yataiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kukusanya na kubakiza Tozo ya Huduma kwa Abiria *(Passenger Services Charge)*, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa pamoja zifanye upembuzi yakinifu kuhusu utaratibu bora wa kukusanya, kubakiza na kutumia Tozo ya Huduma kwa Abiria kwa asilimia 100 kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania; na

b) Kuweka masharti ya kisheria ambayo sasa yataiwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kutumia mapato yatokanayo na Tozo hiyo kwa uhuru na ufanisi zaidi.

### 3.2.2 Usalama wa Abiria na Watumiaji wa Viwanja vya Ndege

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kuthamini jitihada za Serikali katika kusimamia usalama wa abiria na watumiaji wa viwanja vya ndege nchini. Pamoja na hayo, Kamati ina maoni kwamba, uratibu wa masuala ya usalama hususan katika kukabiliana na hatari zitokanazo na majanga ya moto katika viwanja vyetu, unapaswa kuwekewa utaratibu maalum ambao utaiwezesha Mamlaka kutoa huduma hiyo kwa ufanisi zaidi. Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka nyingine yeyote husika, kufanya upembuzi wa kina ili kubaini namna bora za kisheria ambazo zitawezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuwa na Kikosi cha Kukabiliana na Moto na Uokoaji *(Airports Firefighting Brigade and Rescue Service)* ili kuongeza weledi utakaokidhi viwango vya kimataifa; na

b) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuandaa mapendekezo ya kuanzisha Kikosi cha Kukabiliana na Moto na Uokoaji *(Airports Firefighting Brigade and Rescue Service)* na namna ambavyo kitajumuishwa katika Muundo wa Mamlaka kwa namna ambayo itawezesha kuongeza ufanisi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. **Mwenyekiti**
2) Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. **Makamu**
3) Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. Mjumbe
4) Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. Mjumbe
5) Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. Mjumbe
6) Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. Mjumbe
7) Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. Mjumbe
8) Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. Mjumbe
9) Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. Mjumbe
10) Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. Mjumbe
11) Mhe. Geoffrey I. Mwambe, Mb. Mjumbe

12) Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. Mjumbe
13) Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. Mjumbe
14) Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. Mjumbe
15) Mhe. Livingstone Jpseph Lusinde, Mb. Mjumbe
16) Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. Mjumbe
17) Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. Mjumbe
18) Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. Mjumbe
19) Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. Mjumbe
20) Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. Mjumbe
21) Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. Mjumbe
22) Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb.) akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb.), kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada. Vilevile, niwashukuru watendaji wa Wizara ya Uchukuzi, na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius W. Kahyarara kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha Uchambuzi wa Muswada. Aidha, niwashukuru watendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chini ya uongozi wa Mhe. Hamza Saidi Johari, Mb.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameteuliwa hivi karibuni, na kwa kuzingatia kwamba yeye ni mdau wa muda mrefu wa sekta ya anga nchini inayosimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, nitumie fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, kumpongeza kwa kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi hiyo muhimu. Tunamtakia heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
28 Agosti, 2024

**SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati, ahsante sana tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, hapa ninayo majina ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo letu la Kyela lakini kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuiheshimisha Tanzania Kikanda na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunajivunia wewe kama Rais wa Mabunge Duniani, ni kwa sababu Mheshimiwa Rais alisimama na alitengeneza mahusiano Kimataifa, watu na nchi zikatuunga mkono, kwa kweli Mheshimiwa Rais ametupa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunajivunia Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ni kwa sababu Mheshimiwa Rais amesimama yeye mwenyewe kwa kinywa chake na kwa sura yake akimwombea Mheshimiwa Dkt. Ndugulile awe pale alipo kwa sasa. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kuiweka Tanzania kwenye ramani. Haya yanatokea mara chache sana, lakini kwa Rais huyu yamekuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais naomba tuseme, kama ilivyo popote pale na vyovyote itakavyokuwa, Mheshimiwa Rais jina lake litaandikwa kwa kalamu ya wino wa dhahabu duniani na Mbinguni kama itakavyokuwa Mungu atakavyomshushia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mawaziri wetu ambao wanahusika na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kufanya kazi hizi na katika hili leo. Nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Prof. Mbarawa, ni Mwalimu mzuri ambaye amemfanya kijana wake Mheshimiwa Kihenzile ameingia kwenye mfumo haraka kiasi kwamba imekuwa ni tofauti na tulivyotegemea. Ameteuliwa tu na tayari ameingia kwenye mfumo na anafanya kazi vizuri sana. Tunawashukuru sana kwa upacha mlionao na jinsi mnavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria yetu hii naomba tuiunge mkono, na sababu kubwa ni kwamba sheria hii inaenda kuleta sura nyingine kabisa ya umiliki wa viwanja vya ndege na inaenda kutengeneza usalama mkubwa tofauti na ilivyokuwa nyuma. Hapo nyuma kulikuwa na viwanja vingine ambavyo kila mtu alikuwa anaviendesha kwa jinsi anavyojua yeye.

Mheshimiwa Spika, kuna wawindaji wako huko porini walikuwa wanaendesha *airstrips* ambazo hazitambuliki na *TAA*. Leo hii viwanja vyote hivyo vitaenda kuwa chini ya *TAA*. Haya ni mapinduzi makubwa kwenye eneo hili. Nataka niseme tutaenda kupata manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kupitia sheria hii, masuala tena ya *KADCO* yanaenda kufa. Hakuna mtu atakayeleta matatizo yaliyotokea hapo katikati wala atakayelalamika kwa nini sasa kuna *KADCO* halafu kwa nini kuna *TAA?* Hata *KADCO* ikiwepo itakuwa chini ya *TAA*. Kama itakuwa ina manufaa na itahitajika kuwa hivyo, lakini ambaye tutakuwa tunam-*question* atakuwa ni *TAA*.

Mheshimiwa Spika, sheria hii itaimarisha sana utendaji. Kwa maana gani? Kwa maana ya kwamba inaenda kuifanya *TAA* kuwa Mtendaji Mkuu ambaye ana uwezo wa kufanya biashara

bila kuingiliwa na kuingiza kipato. Katika hili tunaomba sana kusisitiza, Serikali ihakikishe inaifanya *TAA* kufanya biashara zake kama kampuni nyingine na wakala wengine. Leo ukienda Shanghai utaikuta Emirates inaendesha *business lounge* na *first class lounge* zilizopo pale Shanghai - China. Tunataka pia *TAA* waimarishwe hizo *lounge* ziwepo mahali popote ambapo wanaenda, nafikiri tutaifanya *TAA* kupata kipato kizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka zaidi, naomba nizungumzie suala la *service charge* ambayo ni pesa ambayo abiria wanalipa kwa ajili ya matumizi ya viwanja vya ndege. Siyo kwamba hatuiamini *TRA,* tunaiamini sana na tunaamini kwamba inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, tunachotaka sasa ni kuishauri Serikali ichukue hili, iwe ni mapato ya *TAA* ili iweze kufanya mambo yake kwa uharaka. Hata kama wako chini ya mwamvuli wa Hazina, lakini pesa yao itunzwe pembeni, waiombe kuifanyia kazi. Matunda ya hii tumeshaanza kuyaona, tumeyaona *TPA*. *TPA* tumewaachia ile *wharfage* imeleta mapinduzi makubwa sana na ndiyo maana ninawasifu hawa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, leo kuna miradi ya ujenzi ambayo ingesimama, kwa mfano mradi wa ujenzi wa Mbamba *Bay*, leo tunaambiwa *TPA* wenyewe kwa fedha hizo tayari wameshalipa fedha za awali kwa Mkandarasi wa kujenga ile bandari. Kwa hiyo, tungeomba hata hawa *TAA* wapewe hiyo fedha ili wawe na uwezo wa kuendesha hivyo viwanja. Tunaona wenzetu wanavyoimarisha mifumo ya usalama kwenye viwanja, wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunaiomba sana Serikali iiache *TAA* iwe inaendesha zimamoto yake. Haiwezekani leo magari na vifaa vyote vya uokoaji ni vya *TAA,* lakini kinachotokea wafanyakazi wanaoviendesha eti ni wa Jeshi la Zimamoto. Hii haikubaliki, katika uwajibishaji inakuwa ni ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mifano mizuri, wenzetu wengi kwenye viwanja wana *brigade* zao. Kwa mfano, wapo wenzetu

wa Austria wanayo *Fire Brigade* yao inaitwa *Betrips Feuer Vayer Salzburger Flughafen.* Ni kitengo chao cha kuendesha haya mambo ya zimamoto. Zambia na India wana *Fire Brigade* yao ambayo ni kitengo ambacho kinaitwa *Airport Rescue and Firefighting.* Pia, wapo Frankfurt na Korea, wana *Airport Firefighting Rescue Unit.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba hata *TAA* waendeshe zimamoto zao kwa sababu hata mafunzo ya uzimaji wa moto na uwezo wa uokoaji, *(preparedness)* ni tofauti na unavyozima nyumba ikiwaka moto. Kwa hiyo, tunaomba hiki kitengo kijitegemee na wawe na uwezo wa kukiendesha ili kuwe na uwezo wa kuwajibishana ili huyu meneja ambaye anaendesha awe na mamlaka ya wafanyakazi wake. Sasa hivi tunamnyima mamlaka yake.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya, naomba Bunge hili lituunge mkono katika Muswada huu. Nami naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

Haya, Mheshimiwa Mwanaisha hayupo, namwita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hoja au Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege ya 2024.

Mheshimiwa Spika, kwanza, unipe nafasi niweze kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kusimamia Serikali yetu ya Awamu ya Sita na kuiongoza nchi yetu sawia na Tanzania iko salama. Kwa hakika sisi kama Wabunge na wananchi tunajivunia yeye kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, ushahidi upo katika maeneo mengi, lakini ni ushahidi tosha kwamba angalau sasa *SGR* ambayo ilikuwa historia sasa tumeanza kuona watu wanatoka Dar es Salaam kuja Dodoma kwa muda wa masaa manne na watu wako *comfortable* kabisa. Ni jambo la kihistoria ambalo kwa hakika lilikuwa ni ndoto na sasa imetimia. Hiyo ni dalili mojawapo ya uongozi thabiti alionao Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi tumeona maendeleo makubwa kwenye majimbo yetu, wananchi wamefikiwa na huduma mbalimbali za kijamii, hiyo kwetu sisi tunajivunia. Katika muda huu wa uongozi wake wa miaka mitatu na ushee tumeona mabadiliko makubwa ya kimaendeleo na kwa kweli uungwana ni vitendo lazima tumpongeze na kumtia moyo sana Mheshimiwa Rais kwamba Watanzania wanamuunga mkono kwa nyanja zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili nachukua nafasi hii kukupongeza wewe kwa kazi kubwa unayoifanya kusimamia Bunge letu Tukufu. Kwa hakika jana baada ya kusimamia lile suala la Malonje, wananchi wengi wamepongeza sana namna ulivyosimamia haki ya wananchi wale na namna ambavyo umeelekeza kupitia Kiti chako kuhakikisha wananchi wale wa Malonje wanaishi salama na kuhakikisha utengemano wa amani na ndiyo maendeleo yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli unaitendea haki nafasi hiyo na kwa hakika ndiyo maana ulipewa Urais wa Mabunge Duniani, kwa hakika unafanya kazi nzuri. Wale watu wa Mbeya tunaendelea kuwaomba, waendelee kuwa na imani nawe, mwakani wakupitishe kwa mwendo wa mserereko ili urudi tena Bungeni uendelee kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao Muswada mbele yetu ambao unakuja kutunga Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kwa kweli kama wengine wanavyosema, ni kwamba kabla ya kuletwa sheria hii mamlaka hii ilikuwa ni wakala tu wa Serikali akifanya kazi kwa niaba ya Serikali katika kusimamia viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na upungufu mwingi uliosababisha kuletwa kwa sheria hii. Hata wakati wa usimamizi wetu kama alivyosema Mwenyekiti wetu kwenye taarifa, tulikuwa na matatizo makubwa katika usimamizi wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia eneo hili pamoja na kuwa leo tunatunga mamlaka hii iweze kusimamia viwanja vya ndege, bado kuna baadhi ya viwanja vya ndege haviko chini ya *TAA*. Naamini kupitia sheria hii itaenda kuboresha usimamizi wa viwanja vya ndege, maana yake itaenda kuondoa tatizo la kiusalama katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, duniani kote pamoja na kuwa mifumo mingine ya usafirishaji, ina usalama na kwenye ndege usalama ni mkubwa zaidi kuliko usafiri wowote. Kwa hiyo, tunapoongeza vionjo hivi, usimamizi huu, tunawahakikishia wananchi na Watanzania na watu duniani kwamba Tanzania ni sehemu salama ya kutua na hivyo watakuja kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati naenda kuchangia kwenye eneo hili, nitachangia maeneo mawili. Eneo la kwanza, kwa mujibu wa *ICAO* ambayo ni mamlaka inayosimamia viwanja vya ndege duniani, ina vigezo vyake inavitoa kila mara na vigezo. Kwa hiyo, kama taasisi haina uwezo mkubwa wa kifedha haitaweza kuwa na ushindani katika viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, leo hii mtu unaweza ukatua katika uwanja wa ndege *A,* ukaenda na uwanja wa ndege *B*, utakuta ni tofauti sana kwa sababu ya huduma zilizoko pale ndani. Kwa hiyo, tukiifanya hii mamlaka ikawa na uwezo wa fedha itaweza kuboresha vigezo kwa mujibu wa *ICAO*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ambalo hata kwenye Kamati tumelisema ni kwamba ni vizuri Serikali ikae kupitia Wizara zinazohusika ikiwemo Wizara ya Fedha ione namna ambavyo itawaachia wenzetu hawa wa *TAA* kukusanya ile tozo ya huduma ambayo inatolewa na abiria iweze kubaki katika taasisi hii ambayo leo tunaenda kuipa mamlaka kamili. Ikiwa na

fedha zake zenyewe itakuwa haisubiri tena suala la kupeleka maombi kwenda Wizara au Hazina ili kupata fedha kutengeneza au kuboresha viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka niombe, ombi letu, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika viwanja vyetu, lakini vinatakiwa viendelee kutunzwa. Kwa hiyo, ombi langu naomba hii *customer service charge* waachiwe watu wa *TAA* ili wawe na uwezo wa kukusanya na kutumia ili kuendana na vigezo vya *ICAO* ambavyo kimsingi ni *standard* ya dunia nzima. Hatuwezi sisi kuwa tumejiweka kama kisiwa na tukajikuta hatuboreshi viwanja vyetu.

Mheshimiwa Spika, hii itaweza kufanya hata baadhi ya *airlines* zisilete ndege katika viwanja vyetu hivyo, tutakosa fursa kubwa ya kiuchumi na sasa hivi tumeboresha suala la utalii, litakuwa limezuia baadhi ya watalii kuletwa katika nchi yetu moja kwa moja. Kwa hiyo, huu ni ushauri wetu kama Kamati na tumesema kwenye Kamati naamini Serikali itaendelea kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba wanawapa *TAA* uwezo huu wa kukusanya fedha hizi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni upande wa usalama wa usafiri wa anga. Eneo hili ni kipaumbele kwa sababu mtu akiwa salama ana uhakika na safari yake. Kwa hiyo, ombi langu nilikuwa nataka niombe, ili kumpa *comfort* mtumiaji kwa maana ya abiria, lazima tumhakikishie usalama wake.

Mheshimiwa Spika, ombi letu lilikuwa ni hilo tu kwamba kumekuwa na mgongano kwamba wenzetu wa *TAA* wana vifaa vyote vya *rescue* kwa maana ya magari ya zimamoto na vifaa vyake. Wamekuwa wakifanya kazi pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba wewe una gari halafu dereva hakuhusu, maana yake ni kwamba huna uhakika kama chombo chako kiko salama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi letu tulikuwa tunaomba kuwe na *Fire Brigade* katika viwanja vya ndege ili kiwe ni kitengo

chao wenyewe, waweze kuwa na mamlaka ya kuwasimamia wale wafanyakazi ambao ni askari wa zimamoto.

Mheshimiwa Spika, leo hii ikitokea mfanyakazi amefanya makosa, Wizara ya Uchukuzi haina uwezo wa kumchukulia hatua yoyote kwa sababu sio mfanyakazi iliyemwajiri. Kwa hiyo, ombi letu, tunaomba ili kufanya usalama na usamamizi uwe mzuri, Serikali ifikirie kuwa na hiyo *brigade* maalum ya kuzuia majanga ya moto katika viwanja vya ndege ikiwa inasimamiwa na *TAA* kupitia Wizara ya Uchukuzi kuliko sasa ikiwa inasimamiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutavutia *airlines* mbalimbali duniani ziweze kuleta ndege zao hapa kwa sababu usalama unakuwa mkubwa na kufanya vivutio vikubwa ikiwemo kuendana na ule utaratibu wa sasa wa kuboresha masuala ya utalii duniani. Ninajua sheria hii ni nzuri na ina manufaa makubwa. Ombi langu kwa Waheshimiwa Wabunge, tuipitishe ili tuwape *TAA* mamlaka kutoka kuwa wakala ili waweze kusimamia vizuri usalama wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono Hoja. Nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko Mezani. Kama walivyosema wenzangu, nami nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na utaratibu wa kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais utaendelea tu kwa sababu tunaendelea kupata mazuri na sisi lazima tuendelee kushukuru kwa sababu hiyo ni sifa kubwa ya ubinadamu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru tena na tena kwa sababu utakumbuka katika Mkoa wetu wa Morogoro na hasa Jimbo letu na Wilaya yetu ya Kilombero tulikuwa na malalamiko makubwa

ya barabara yetu ya lami ya Ifakara – Kidatu na mambo mengine makubwa. Tunashukuru kwa sababu lile jambo limekamilika. Kama tulisimama katika Bunge lako, wengine tukatamani mpaka kukaa chini wakati tunaanza Bunge mwaka 2020, 2021 tukisimama hoja ni Barabara; Mheshimiwa Rais ameleta fedha.

Mheshimiwa Spika, leo umekuja kule unaenda mpaka Mlimba kule umemjengea nyumba Mtanzania ambaye hana uwezo, tumefurahi sana, Mwenyezi Mungu akubariki. Umeona barabara ile kutoka Mikumi – Ifakara, sehemu ilikuwa inatumia masaa matatu, lakini sasa hivi ni nusu saa, unateleza unafika Ifakara Mjini. Kwa nini tusimshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na mambo yangu matano, karibu sita, yote yamekamilika. Mradi wa maji tumepata, sekondari tumepata na kadhalika. Nawashukuru sana wananchi wetu kwa kutuunga mkono. Tuna changamoto kubwa sana ya barabara za mitaa, tunaendelea kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hapa niseme, wasemaji hawaishi. Wewe unafanya mambo makubwa pale Mbeya lakini wasemaji hawataisha. Wasemaji hawa hawajawahi kwisha. Ubaya wengine ni wale wale walimsema Nyerere, ameunganisha nchi bila mkataba; walimsema Mzee Mwinyi; wamemsema Mzee Mkapa; wamemsema Mzee Jakaya; wamemsema mpaka Marehemu Dkt. Magufuli, amefariki sasa hivi wanamsema, na bado wataendelea kumsema Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli ameonyesha utulivu mkubwa wa kuongoza nchi yetu na kuachana na changamoto nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais anawapuuza na anaendelea na kazi ya maendeleo ya nchi yetu, wameachana na Rais Dkt. Samia, sasa wanahamia katika familia ya Rais. Yaani familia ya Rais imekuwa ajenda katika vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie, kwa hali hiyo, tutaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, vyovyote itakavyokuwa, anayechukia achukie, potelea mbali. Hawa hawa

ndio waliosema mabehewa yamekuja mabovu, uuzi mmoja nimesafiri naye kwenye treni, kalala kwenye treni, kasinzia usingizi, lakini leo watu wamesahau mabehewa yameshuka hapa wanasema mabehewa *fake* yametoka Korea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lao watu hawa wanasahau. Juzi kuna mmoja nitakutumia picha, kasinzia anakoroma kwenye *royal class* ya treni. Kwa hiyo, tunampa moyo Mheshimiwa Rais na tunamwambia aendelee na kazi kwa sababu wengine wanasema, wengine mpaka vitu vitokee ndiyo watakuja kuviona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kwenda kwenye mada. Hoja ya Kamati naiunga mkono na kwa kweli naunga mkono hoja za wadau. Nimesoma katika Kamati ya Miundombinu, wadau wa usafirishaji wametoa maoni yao na sisi tuliyasikiliza kwenye Kamati, tumeyasoma, naunga mkono hoja ya kutungwa kwa sheria hii ya mwaka 2024. Kwa nini tunaunga mkono hoja?

Mheshimiwa Spika, tunaunga mkono hoja ili kuweka mifumo ya kisheria ya usimamizi, uendeshaji na uanzishaji wa viwanja vya ndege. Katika uendeshaji na usimamizi wa viwanja vya ndege, kuna changamoto mbalimbali na sisi kama Kamati tumetembelea viwanja vya ndege katika maeneo ya ndani na nje ya nchi. Sasa Waheshimiwa Wajumbe hapa wamesema, mimi nataka kusisitiza suala moja la uokoaji na usalama katika viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika sheria za kimataifa, jambo hili ni kama linapewa mkazo zaidi. *ICAO,* taasisi ya Kimataifa inayosimamia viwanja vya ndege imekuwa ikishtukiza mara nyngine ili kuvipa *standard* viwanja vyetu vya ndege kwa maana kwamba wanaweza wakatoa taarifa kwamba sehemu fulani moto unawaka, wanaweza wakatoa taarifa kwamba jambo fulani linatokea sehemu fulani na baadaye wapime uwezo wa nchi yetu katika kuokoa na kuzima moto katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, sasa kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa sababu ya mwingiliano wa Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto lina historia nzuri chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, chini ya Mheshimiwa Waziri, wanafanya kazi kubwa sana lakini tuna mfano wa moto uliotokea Bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, pale Mamlaka ya Bandari walipokwenda kuhojiwa na sisi kama Kamati, ilionekana kwamba askari (dereva) wa gari ya zimamoto alikuwa amepangiwa majukumu mengine na kiongozi wake ambaye wanatawaliwa kijeshi. Ndiyo maana Kamati inaleta hoja hii kwamba kuwe na kikosi maalum chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambacho watakisimamia, wataweza kuwawajibisha na kutumia bajeti ya viwanja vya ndege katika kuboresha uzimaji moto na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *TAA* inanunua gari la zimamoto *1.5 billion shillings* lakini linanunua kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto ambalo liko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, sisi kama Kamati tumeshauri na tunasisitiza, wao ni wataalamu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Waziri wa Uchukuzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wengine wakae waone utaratibu gani mzuri wa kutengeneza kikosi ambacho Mkurugenzi Mkuu wa *TAA* anaweza kutoa maelekezo kukiboresha kutokana na bajeti yake. Hili ni jambo la msingi sana, litatupa *standard* nzuri sana katika kumiliki viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Spika, pili, viwanja vyetu vya ndege vinajiendeshaje? Tumeona Mheshimiwa Rais akijaribu kueleza umuhimu wa hizi taasisi na hizi mamlaka za Kiserikali kujitegemea na ikibidi mpaka kutoa tozo za Serikali. Sasa juzi kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe, tumefanya katika *wharfage* ya bandari na Mkurugenzi wa Bandari amekuja kwenye Kamati, ametoa matunda ya jambo hilo kwa mwezi mmoja tu. Mpaka juzi wanaanza kusaini bandari ya makaa ya mawe kule Mtwara, jambo hili halikuwepo. Ndiyo maana tunasema katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, waruhusiwe kukusanya ile tozo ya abiria ili irudi kwenye *TAA*.

Mheshimiwa Spika, abiria ukipita kwenye viwanja vya ndege upate huduma nzuri kutokana na ule mchango unaoutoa. Sasa ikishaenda huko, Wizara ya Fedha wana mahitaji mengi. Tunataka vituo vya afya, vituo vya Polisi, mpaka ije irudi huku unakuta picha inapigwa katika jengo la kiwanja cha ndege panavuja, *management* ya viwanja vya ndege wanasubiri wapate *OC* kutoka Serikalini wakati wao wana tozo wanakusanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasisitiza sana kwamba tozo hii ilikuwepo katika sheria ya 1962. Mwaka 2005/2006 Mheshimiwa Waziri anayehusika wakati huo akairudisha, akaelekeza iende *TAA* na baadaye Wizara ya Fedha ikawa inapeleka tozo hii *TAA* kama *retention*. Mwaka 2017 tukapitisha sheria tukabadilisha, tukafuta *retention* katika mamlaka ya umma. Kwa hiyo, tunaomba sasa sheria hiyo ipitiwe upya hizi fedha za tozo ya abiria zirudishwe *TAA* kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, sisi Ifakara tuna kiwanja cha ndege, maboresho hakuna. Dar es Salaam pale wenyewe jengo la *Terminal Two* shida tupu; nenda Mtwara, nenda Lindi, tumetembelea viwanja vya ndege vina hali mbaya. Imani yetu, kwa mujibu wa sheria, *TRA* ikikusanya itumie fedha hizi kwa mujibu wa mwongozo na mamlaka ya kisheria ili tuweze kupata viwanja vya ndege vyenye ubora, endelevu na tuanzishe vingine.

Mheshimiwa Spika, tumefika pale Mbeya tumeona bado kiwanja chako cha ndege cha Mbeya kinataka maboresho. Tunataka Mtwara pale paboreshwe. Kwa hiyo, tozo hii itasaidia sana, nami naomba kuunga mkono hoja kusisitiza tupate kikosi cha zimamoto katika viwanja vya ndege, tozo hii irudishwe kwa *TAA* ili iweze kujiendesha na siku moja tunavyosafiri huko duniani tukishuka pale *airport* yetu iwe sawa na *airport* nyingine. *Scanner* ikiharibika tu pale foleni. Juzi tumeshuka hapo foleni, lakini utaratibu ukiufuata utaambiwa mchakato wakati wao wana tozo yao.

Mheshimiwa Spika, wewe unasafiri duniani, wewe ni Spika wa Mabunge ya Dunia, utakuwa mtu wa kwanza humu kuongoza

kutembelea *airports* mbalimbali. Katika hizo *airports,* watu wameshaachana na habari ya kuvua mikanda *airport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wanashona suruali kubwa, mtu anavua mkanda, anashika suruali hivi na begi lake anapita. Haya mambo ya teknolojia ya zamani, tozo hii irudishwe *TAA* wanunue mashine za kisasa. Mtu unapita na begi lako na vitu vyako, wakiwa na tatizo na wewe wanakwambia kaa pembeni, tunaku-*search*. Sasa mashine zetu bado za zamani kwa sababu mapato yetu yanakusanywa pamoja, yanapangiwa matumizi mengine tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunataka *TAA* ipate fedha hizi iboreshe *standards* zetu za *airports* zifanane na dunia nyingine. Hata hali ya hewa ya *airport* ukishuka Dubai, ukishuka Dar es Salaam ifanane. Hata wewe unavyoenda Marekani, juzi nimekuona uko huko unatuwakilisha, unaona *airport* zao, ukishuka huku hali inakuwa tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nimesisitiza mambo hayo mawili. Ahsante sana, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani. Kwanza kabisa naanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kwa kweli ununuzi wa ndege umeweza kutupa sifa kubwa sana katika nchi yetu. Pia ujenzi wa viwanja bora katika nchi yetu ametupa sifa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kukupongeza sana wewe Spika wetu ambaye toka umekuwa Rais wa Mabunge ya Dunia umeweza kuing'arisha nchi. Tanzania sasa imeanza kuonekana kimataifa na hata ukitembea katika ndege ukiulizwa, wewe ni Mbunge wa wapi? Nasema Rais anakotoka mimi ndiyo Mbunge wa nchi hiyo. Kwa hiyo, unatufagilia sana na unatisha. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ambaye leo hii ametupa heshima kubwa sana. Sisi tunaamini kwamba wewe ndiwe uliyeifungua njia hiyo ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile naye leo hii ameendelea kutuletea sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Mheshimiwa Prof. Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile Naibu Waziri wa Wizara hii ya Uchukuzi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi pamoja na Kamati ambayo imeweza kutuletea hapa Bungeni, Kamati ya Miundombinu pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hii Sheria ya Viwanja vya Ndege ya kuipa mamlaka jukumu la uanzishaji, uendelezaji na usimamizi wa viwanja hivi vya ndege nchini. Naendelea pia kuipongeza Serikali kwa ununuzi wa ndege nchini Tanzania, Bara na Zanzibar na kwa kuona umuhimu. Hii imechangia sana utalii katika nchi yetu. Tumeona jinsi Mheshimiwa Rais alivyotangaza utalii. Tukipitisha sheria hii nadhani utalii utatupatia kipato kikubwa sana nchini, Tanzania na Zanzibar pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa ndege ni jambo lingine na ujengaji wa viwanja vya ndege vya kiwango ni muhimu. Kwa hiyo, sheria hii itaendeleza uhalisia wa kuwa na ndege za kutosha na kuipa nguvu mamlaka ya viwanja kuendesha kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la kurudisha hii *Passenger Service Charges* ni la msingi. Mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati hii. Muda mrefu sana tuliomba hii *Passenger Service* warudishiwe mamlaka ili iweze kuwasaidia katika ujenzi na kuendeleza.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia kwamba kuna vitu ambavyo wanatakiwa wafanye kwa haraka vinakuwa havifanyiki kwa haraka, kwa hiyo, wakirudishiwa hii *Service Levy* itasaidia kufanya maboresho makubwa sana katika uendeshaji wa shughuli zao za kila siku na kuhakikisha kwamba sasa hivi mamlaka inajiendesha

kwa ubora zaidi. Kwa hiyo ni muhimu sana Serikali ikairuhusu *charges* hizi kuendeshwa na *TAA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hii ni muhimu sana, itasaidia kuimarisha usalama pia katika viwanja vya ndege, na pia kama viwanja vya ndege nchini vitakuwa kwenye umiliki wa *TAA*, usimamizi kwao utakuwa ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, sheria ile itasaidia sana kuwa na miundombinu na kuwa na magari ya zimamoto, kama walivyosema wengine, yatasaidia kuliko sasa hivi ambapo magari ya zimamoto yapo kwenye Wizara nyingine, lakini kama magari ya zimamoto yatakuwa chini ya *TAA*, itasaidia kwa sababu wakati wowote ambao yatahitajika, yatatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona magari mengi ya zimamoto kwenye viwanja vingi zinakuwa hayapo au yanakuwa yameharibika. Kwa hiyo, tukiwa na hii sheria itasaidia sasa vifaa vingi muhimu, *TAA* itaweza kujiendesha yenyewe lakini pia mifumo madhubuti, thabiti kisheria na usimamizi itasaidia sana katika sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niendelee kupongeza kwamba katika Mkoa wetu wa Iringa tunacho kiwanja chetu cha ndege ambacho kwa kweli kimeboreshwa sasa hivi kama 93%; na tunashukuru sana Mheshimiwa Rais alikuja kukizindua. Vilevile alipokizindua, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja mwezi wa Saba kutembelea katika kiwanja cha ndege na aliwaambia *TAA* kwamba wawasiliane na shirika la ndege ili ndege iweze kutua.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua, wakati tunapitisha hii sheria, tarehe 01 Septemba walisema ndege ya *ATCL* itue pale Iringa. Tunajua kwamba sasa hivi Iringa na Nyanda za Juu Kusini utalii unapamba moto. Tunategemea kwamba kwa kutumia Sheria hii, tunakwenda hata katika Nyanda za Juu Kusini. Ndege zitakapotua katika Mkoa wetu wa Iringa, itasaidia sana utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba lile agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wanakwenda kujibu haya majibu watuambie, tarehe moja ni wiki ijayo, ndege itatua? Kama haitatua tunaomba tujue kwamba maagizo yakitolewa na viongozi wakuu huwa hawafanyii kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *TAA* leo hii tunapitisha hii sheria ambayo nami naunga mkono kwa asilimia mia moja, tunaomba maagizo yakitolewa hasa kwa viawanja vya ndege, basi yafanyike kwa haraka ili sasa iweze kusaidia. Tunapopitisha sheria hizi kwa mafanikio na ufanisi mkubwa tuhakikishe kwamba viwanja vya ndege na ndege hizi zinasaidia utalii nchini ili sasa tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, pia tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye amefanya matangazo kupitia utalii kwa kiasi kikubwa sana ili nchi zote ziweze kuja kutua na utalii uendelee katika nyanda za juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mbarawa aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru tena Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana tena na kujadili hoja hii iliyowasilishwa muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi. Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa wawazi na kutoa michango yao ya kina wakati wa kujadili hoja hii. Nithibitishe kwamba michango yao yote tumeichukua kwa uzito mkubwa na tunakwenda kuifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba sekta ya anga inakua kwa mujibu wa mipango tuliyoiweka.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Suleiman Moshi Kakoso na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kwa hoja nzuri zilizotolewa na Kamati yao. Nakiri kwamba hoja hizi ni muhimu sana kwa maendeleo na ukuaji wa miundombinu na huduma za usafiri wa anga hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya na uongozi wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufafanuzi wa kijumla na mfupi kuhusu hoja mbalimbali zilizowasilishwa. Kama nilivyosema wakati nawasilisha hoja hii, lengo la kutungwa kwa sheria hii ni kuweka mfumo madhubuti na thabiti wa kisheria wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada huu unakusudia kutatua changamoto mbalimbali za usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege ambapo hapo zamani ilipokuwa Wakala wa Viwanja vya Ndege ilikuwa *TAA* inakumbana nazo. Pia kuna changamoto nyingi ambazo leo zinaukabili usafiri wa anga. Kwa mfano, kumekuwepo na changamoto kwenye usimamizi wa viwanja vya ndege, kumekuwa na ubadilikaji wa kila mara wa Kanuni na usafiri wa anga na itifaki za usalama duniani.

Mheshimiwa Spika, leo ukienda kwenye viwanja vya ndege, kama alivyosema, unaambiwa uvue viatu, ufanye nini, ni kwa vile kulikuwa na hayo mabadiliko na yataendelea kuwepo kulingana na jinsi teknolojia inavyokua. Tunaamini kwamba changamoto hizi zote zitaweza kutatuliwa na sheria hii. Sheria hii inayopendekezwa pamoja kanuni na miongozo, itawezesha usimamizi mzuri wa viwanja vya ndege hapa nchini pamoja na uboreshaji wa usalama katika viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Spika, pia kuna changamoto, kuna matarajio makubwa ya abiria wanaotumia huduma za ndege, kuanzia wanapoingia kwenye viwanja vya ndege, wanapopanda ndege na mpaka wanapopokea mizigo yao. Sasa hivi abiria anataka akishuka tu kwenye ndege, mzigo wake aukute pale. Haya yote yanaweza kukamilika au kutatuliwa kama tutakuwa na sheria, kanuni, na miongozo mizuri.

Mheshimiwa Spika, kama tutaweka mifumo mizuri ya kigitali, tunaamini kwamba abiria watapata huduma bora na huduma ambayo imetukuka. Kwa hiyo, sheria hii ni muhimu, na tunaamini kwamba sheria hii itaweza kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo kubwa la miundombinu. Kama tunavyofahamu, upanuzi au uboreshaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege kunahitaji uwekezaji mkubwa. Changamoto hii ya kupata fedha na ujenzi wakati wa utumiaji wa viwanja vya ndege, iko haja ya kupata sheria ambayo itashirikisha kwa kiasi kikubwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba ushirikishwaji wa sekta binafsi ambao sheria hii inapendekeza, utaweza kuboresha huduma za usafiri wa anga hapa nchini, utaweza kuboresha utendaji wa sekta ya anga hapa nchini, na utaweza kuboresha huduma ya uendeshaji wa viwanja vya ndege. Tunaamini kwamba baadhi ya viwanja vya ndege tukishirikiana na sekta binafsi, huduma zitakuwa nzuri na wananchi watapata huduma ambayo ni bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye maeneo mawili ambayo Kamati pamoja na wachangiaji wote wamewasilisha hapa. Eneo la kwanza ni eneo la kitengo cha zimamoto. Tunakubaliana na Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kuhusu jambo hili. Kama Kamati ilivyosema, tutakaa sisi Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Ulinzi halafu tutafanya upembuzi yakinifu kuona jinsi gani jambo hili tutaweza kulisimamia

Mheshimiwa Spika, lakini tunaomba Waheshimiwa Wabunge wasisahau kwamba maoni ya Tume ya Hakijinai ilielekeza kwamba Idara ya Zimamoto sasa ipelekwe huko halmashauri, kwa vile tutakaa pamoja sote tuone tutalifanyaje jambo hili kwa maslahi mapana ya usalama wa viwanja vya ndege hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa sana ni kuhusu *Passenger Service Charges*. Kama Kamati ilivyoeleza na Waheshimiwa walivyozungumza, Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tutakaa pamoja, tuzungumze jambo hili tuone jinsi gani ambavyo tutaweza kulitatua ili *service charge* hiyo iweze kubaki kwenye viwanja vya ndege. Ninavyozungumza sasa hivi, *service charge* kwa mwaka ni takribani shilingi bilioni 70.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo Serikali tumewekeza fedha nyingi kwenye kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege hapa nchini. Kwa mfano, Uwanja wa Msalato ambao kuna *Phase I* na *Phase II*; *Phase 1* ni ujenzi wa *runway*, na *Phase II* ni ujenzi wa jengo la abiria. Tunatumia takribani shilingi bilioni 360, na uwanja huo hasa ile *runway* tunategemea mwezi Oktoba utakamilika na tutaanza kufanya safari za ndege kupitia Kiwanja cha Ndege cha Msalato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha, kwa mfano Uwanja wa Ndege wa Musoma tumetumia au tunaendelea kutumia takribani shilingi bilioni 36.63; Shinyanga tunatumia takribani shilingi bilioni 49.197; Iringa kama alivyosema Mheshimiwa Ritta, pale tumetumia takribani shilingi bilioni 63. Huko Songwe tumejenga jengo zuri la abiria na tumetumia takribani shilingi bilioni 28.87; huko Mtwara, uwanja wa ndege tayari *Phase I* tumeshatumia taribani shilingi bilioni 56.993.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaenda kujenga jengo la abiria ambapo tutatumia takribani shilingi bilioni 70 na mkandarasi tumeshampata. Huko Lindi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakwenda kujenga *runway* pamoja na jengo la abiria ambapo tutatumia takribani shilingi bilioni 130.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Serikali tunatumia takribani shilingi trilioni 1.1 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege hapa nchini. Niendelee kusema tena kwamba tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati yetu na tutakwenda kukaa ili tuweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba tena kutoa hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024**

**MWENYEKITI:** Haya, tuendelee.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jina Refu lina mabadiliko ya Serikali.

Jina Refu

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jina refu la sheria hii lina mabadiliko ya Serikali, wanaongeza neno “uanzishaji”

ambalo halikuwepo hapo. Sasa kwenye haya marekebisho, wakati huo huo wameleta lile jina refu linguine. Liko wapi? Hilo hapo; haya, ngoja kidogo Waheshimiwa.

Mheshimiwa Waziri, hili jina refu, hapa Kiswahili kidogo nilishawahi kusema huko nyuma, kwa hiyo, lazima niseme tena, kwamba utungaji wa sheria kwa lugha ya Kiswahili bado kuna changamoto kidogo inayomkumba Spika, lakini inabidi tuendelee kufanyia kazi.

Kwenye hili jina refu, tumesema, "Sheria ya Kuweka Masharti Madhubuti ya Uanzishaji…" na hayo sasa yanayoendelea. Hivi hii ni Sheria ya Kuweka Masharti Madhubuti au Sheria ya Kuweka Mfumo Madhubuti? Ili tuwe tumetumia Kiswahili ambacho kimekaa sawa, ni kwa ajili ya kuweka masharti madhubuti au kwa ajili ya kuweka mfumo madhubuti?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri "mfumo" ni neno sahihi kuliko "masharti," labda wataalamu wa Kiswahili watusaidie zaidi.

**MWENYEKITI:** Eeh, tusaidiane jamani, mfumo madhubuti au masharti madhubuti? Kama tungekuwa tunayasema maneno haya kwa Kiingereza tungesemaje? Masharti Madhubuti au Mfumo Madhubuti? Wataalamu wako wapi jamani? Humu ndani hatuna wataalamu wa Kiswahili wala wa Kiingereza?

Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili mimi sijui sana, lakini nadhani "Mfumo Madhubuti" ndiyo itakuwa sahihi zaidi.

**MWENYEKITI:** "Masharti" kwa Kiingereza huwa tunaita nini?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *conditions*.

**MWENYEKITI:** Ehe, halafu mfumo! Pengine kwa Kiswahili litaitwa jina tofauti badala ya *system* kwa sababu ni lugha ya

kisheria. Nadhani kuna neno fulani hivi huwa tunatumia tukitaka kusema mfumo, sina hakika kama tunatumia neno *system*.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nafikiri mfumo linakuwa ni neno la Kiswahili linalokaa vizuri kisheria kuliko masharti. Humu ndani tunaweza kukutana na masharti, lakini hii sheria kwa ujumla inaweka mfumo madhubuti wa uanzishaji; si ndiyo, ama! Tusaidiane jamani, tuko katika kutunga Sheria hapa.

Sina simu yangu hapa, ninyi mna simu zenu, hebu angalieni huko, itakaaje vizuri? Pia ni kwa sababu hii sheria tuliyoitunga wenyewe ni lazima ikatafsiriwe Kiingereza. Sasa ile tafsiri itakapokuja tusije tukaiweka katika sura ambayo haitakuwa imekaa vizuri sana. "Masharti Madhubuti" ukitazama huko kwenye simu zenu inasemaje? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuangalie "masharti Madhubuti" halafu "mfumo Madhubuti" au ni "Sheria ya Kuweka Mfumo wa Uanzishaji, Uendelezaji..." bila neno "Madhubuti." Au neno "Madhubuti" ni lazima liwepo? Hebu tutazame kwa haraka haraka.

Waheshimiwa Wabunge, mmeshalipata? Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, inasema *strict conditions,* ndiyo masharti Madhubuti. Sasa sijui kama…

**MWENYEKITI:** Inasema *strict conditions.*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, inasema *strict conditions.*

**MWENYEKITI:** Haya, hebu angalia mfumo madhubuti. Itakuwa *strong system!*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, *strict system.*

**MWENYEKITI:** Inasema!

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ni *strict system*.

**MWENYEKITI:** Sasa nadhani nia ilikuwa ni kuweka mfumo unaotosheleza. Hebu angalia neno *comprehensive* linaitwaje kwa Kiswahili?

Waheshimiwa Wabunge, sasa wakati hili linatazamwa, hili Jina Refu ngoja tutafute maneno mazuri ya kuyaweka hapa, lakini tuendelee, tutalirejea Jina Refu la huu Muswada au limeshapatikana! Ehe, Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nazungumza kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu na kuniteua kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kukupa ile *English version* ya sheria hii ambapo kule tumesema kwamba, ni "*an act to make provisions for effective development, management, operations and maintenance of airports.*" Kwa hiyo, hapa dhana…

**MWENYEKITI:** Hebu soma tena.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** "*an act to make provisions for effective development, management, operations and maintenance of airports, establishment of the Tanzanian Airport Authority and provide for functions and powers and other matters related thereto.*" Kwa hiyo, *gist* ni ku-*make provisions* ambazo zitasababisha kuwa na *effective development*.

**MWENYEKITI:** Sawa. Shida iko kwenye hili neno *effective,* kwa sababu, hapa kwenye marekebisho ambayo mmeleta Serikali, maana yake tukitunga itaitwa *effective establishment* kwa sababu, mmeleta neno uanzishaji hapa. *What is effective establishment? What is effective development?* Si ni *establishment, development* na hayo mengine yote yaliyotajwa,

hilo neno *effective* hapo linakuwa kwenye sheria haliwi *superfluous?*

Waheshimiwa Wabunge, maana yake hili neno *effective* tukalitafutie mwenzie. Hatuwezi kuwa na *effective establishment,* lazima tuliache hapa mwanzo. Maana yake ni hapo mwanzo pawe na Sheria ya Kuweka Mfumo wa Uanzishaji na nini na nini, halafu twende huko kwenye usimamizi, labda ndiyo usimamizi *effective,* lakini haya mengine huku nyuma yanakuwa hayahusiki na hili neno madhubuti kama ni lazima liwepo. Hakuna umadhubuti kwenye kuanzisha jambo. Tuendelee kulifikiri wakati sisi tunaangalia hivi vifungu vingine, tuendelee kulitazama. Wakati tunapitisha vifungu, Mheshimiwa Waziri tazama.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali endelea kuangalia hii *Long Title* isomeke namna gani ili wakati wa tafsiri isije ikaleta changamoto.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu, zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Ibara ya 3 ina marekebisho ya Serikali, wanaongeza maneno hapo "au kupanga kuingia." Kitendo cha uvamizi kinyume cha sheria maana yake ni kitendo cha kuingia au kupanga kuingia mahali au eneo lisiloruhusiwa au kuingilia taratibu za utendaji.

Hili sioni kama lina shida, labda tu Mheshimiwa Waziri unaweza kufafanua kidogo kwa sababu hapa tunaongelea kitendo cha uvamizi. Sasa ni uvamizi gani unaoweza kuwa ndani ya sheria? Si uvamizi ni kinyume tu cha sheria! Hapa tumesema tunafafanua kitendo cha uvamizi kinyume cha sheria, kuna uvamizi unaoweza kufanywa kwa kufuata sheria, ama wote ni uvamizi tu? Kuna haja ya kusema kitendo cha uvamizi kinyume cha sheria? Tunaweza kuwa na uvamizi ambao umefuata sheria?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishafanya uvamizi maana yake umeenda kinyume cha sheria *automatically* kwa sababu, kama siyo uvamizi, umeruhusiwa kisheria. Unaweza kwenda, lakini *once* ikija uvamizi, maana yake tayari umeshafanya kosa. Kwa hiyo, nafikiri tutaiangalia kuweka vizuri.

**MWENYEKITI:** Aah, ndiyo tunaiangalia hapa sasa hivi. Kwa hiyo, haya maneno kinyume cha sheria ni lazima yawepo ili ndiyo uitwe uvamizi? Ama ni kitendo cha uvamizi, halafu maana yake mmeshaweka hapo mbele?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema inaweza kujitosheleza.

**MWENYEKITI:** Haya maneno yanakuwa kwenye sheria yanaitwa *superfluous.* Naona Wanasheria wameshika tama pale. Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, haya maneno yawepo au yasiwepo?

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu yasiwepo, hayaongezi chochote.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana. Kitendo cha uvamizi maana yake ni kitendo cha kuingia au kupanga kuingia na namna hiyo. Kwa hiyo, kwa sababu, ukishasema kuvamia, tena ndiyo kuvunja kwenyewe sheria. Kwa hiyo, hayo maneno yanaondoka hapo.

Kifungu cha Tatu pamoja na marekebisho ya Serikali na marekebisho yaliyofanywa sasa hivi na Bunge, kinaafikiwa?

*(Ibara ya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MWENYEKITI:** Ibara ya Nne haijaafikiwa Wabunge? Maana hakuna aliyeitika.

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

**MWENYEKITI:** Ibara ya Nane, ngoja. Kabla hatujafika ya nane. Hiki Kifungu cha 06 kimeshapitishwa, lakini haya maneno ya pembeni ambayo kwenye tafsiri ya sheria huwa ni maneno ya kuongoza tu na yenyewe tafsiri yake italeta shida kwa sababu tunasema mamlaka ya mamlaka.

Sasa ukitafuta haya maneno yake kwa Kiswahili, hatuwezi kusema maneno “mamlaka ya mamlaka.” Ni aidha, tusema madaraka ya mamlaka au tuseme nguvu ya mamlaka, lakini hatuwezi kuweka mamlaka na mamlaka hapo hapo kwa sababu, moja, inataka kusema *authority* nyingine inataka kusema *power of the authority,* si ndiyo?

Waheshimiwa Wabunge, sasa lile neno *power* haliwezi kutafsiriwa kama *authority* hapa, yaani *authority, authority*. Tutafika tu mahali, lakini naona mamlaka ya mamlaka kidogo inakuwa haijakaa sawa. Kwa hiyo, ni aidha, tutumie neno madaraka ama tutumie nguvu. Kwa hiyo, nguvu inaweza kuwa kwa kiswahili chake labda ni itaitwa *colloquial*? Tutumie madaraka.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie neno madaraka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, vyote viwili kwenye Kiswahili unaweza ukasema madaraka au nguvu, lakini sasa ni lazima utafute neno mojawapo ambalo litakaa Kisheria zaidi kuliko lingine. Kwa hiyo, litakalokaa kisheria zaidi huenda ni madaraka kuliko nguvu, si ndiyo. Kwa sababu, nguvu ni kama vile unavyosema matumizi ya nguvu, sijui naeleweka? Yaani kwenye tafsiri ya kisheria ukisema mtu ametumia nguvu, sio yule anayetumia Madaraka. Tumeelewana?

Kisheria matumizi ya nguvu ni tofauti na matumizi ya madaraka. Tukitumia neno madaraka linaweza kukaa vizuri zaidi hapa kuliko kuitwa mamlaka ya mamlaka. Kuna tatizo hapo Waheshimiwa?

Waheshimiwa Wabunge, hata kwenye Kiingereza hatuiti *authority of the authority,* tunaita *powers of the authority*. Si ndiyo jamani?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa hii *power* ya hapa Kiswahili chetu ili kikae vizuri tutumie Madaraka. Tunakubaliana? Au kuna Kiswahili hakijakaa sawa naona, kuna wataalamu wamefanya kikao kule nyuma. Eti ni madaraka au ni nguvu? Madaraka eh?

Naona hapa tutapiga kura sasa hivi. Haya, wale wa kikao kidogo kule nyuma ni madaraka ama nguvu? Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kikao hiki kidogo, sisi tunaona kwamba nguvu ya mamlaka ndiyo inaweza ikawa sawa, kwa sababu madaraka kwa tafsiri ya moja kwa moja mimi sio mswahili sana, lakini madaraka yanakuwa yanazungumzia kama *ranks* ndiyo madaraka. Kwamba, ulikuwa Koplo sasa umekuwa *Sergeant,* ndiyo tafsiri ambayo naiona ya haraka ya neno madaraka. Kwa

hiyo, hapo mimi nafikiri kama kwenye sheria haiwezi kuathiri, neno nguvu linafaa kutumika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Jamani kamusi ya Kiswahili, hee! Haya Mheshimiwa.

**MHE. BAL. LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukatumia uwezo wa mamlaka.

**MWENYEKITI:** Uwezo. Tutakapotafsiri kwenye Kingereza bado tutatumia neno *powers* au tutatumia *ability*?

**MHE. BAL. LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *power of the authority.*

**MWENYEKITI:** Uwezo…

**MHE. BAL. LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa mamlaka.

**MWENYEKITI:** *Ability* kwa Kiswahili inaitwa nini?

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa mamlaka.

**MHE. BAL. LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uwezo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mbunge wa Muleba.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ukisoma zile sheria zenyewe huwa tunatumia mamlaka ya mamlaka, lakini kwa Kiingereza ni maneno mawili tofauti. Kwa Kiswahili mimi napendekeza libaki mamlaka ya mamlaka ni maneno mawili tofauti ukilisoma vizuri, ingawa kwenye Kiingereza ni maneno mawili tofauti, lakini kwa Kiswahili ni neno moja tulilonalo. Kwa hiyo, napendekeza ibaki mamlaka ya ile mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiweka 'uwezo', ni mambo mawili tofauti. Ukiweka '*ability',* ni maneno mawili tofauti, lakini tulichokilenga pale ni mamlaka ya ile mamlaka.

**MWENYEKITI:** Haya, eeh Mheshimiwa Abdullah.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tafsiri tutafsiri maana na siyo neno na madaraka. Kwa jinsi ilivyokaa unaweza ukaitafsiri kwa *powers of authority*. Sasa ninavyoona "madaraka ya mamlaka" imekaa vizuri zaidi kushinda kutumia neno 'nguvu.' Japokuwa maneno yamefanana, lakini tafsiri yake kwa Kiswahili inakuwa tofauti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa 'madaraka' Kamusi inasema. "mamlaka anayopewa mtu au nchi kufanya au kuamua mambo." Neno lingine mnataka nitafute ni lipi?

**MBUNGE FULANI: '**Nguvu.'

**MWENYEKITI:** Haya, maana ya neno 'nguvu'?

Tuelewane jambo moja, ndiyo maana nilisema maneno mawili haya, 'madaraka' ama 'nguvu' kuna Lugha ya Kisheria. Kwa hiyo, lazima utafute neno ambalo linakuwa na maana tunayoitaka. Kwa sababu, tunatunga Sheria ya Kiswahili, linakuwa na…

**MBUNGE FULANI:** *'Power'*

**MWENYEKITI:** Siyo. Eti linakuwa na *'power'! (Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, linakuwa na muktadha wa Lugha ya Kisheria. Kwa hiyo, lazima tutunge Sheria hata kama ni Kiswahili hatuwezi tu kuweka neno, kwa sababu lina maana fulani, lakini tunaweka neno ambalo litakuwa na muktadha wa Lugha ya Kisheria.

Mheshimiwa Mbunge umesimama.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama niseme kwamba, tuwe *consistent*. Katika ile Sheria ya Manunuzi ya Umma tulitumia *powers of the authority* na ikawa "madaraka ya mamlaka." Kwa hiyo, kwa *consistency's sake, let us use the same* madaraka.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kukumbuka. Huu mjadala unaishia hapa. Tutatumia neno "Madaraka ya Mamlaka." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha 6 kwa sababu, tulikuwa tumeshakipitisha tunabadilisha maneno ya pembeni, lakini na pale kwenye kueleza itakuwa ni "mamlaka" itakuwa na "Madaraka ya kumtaka." Hayo maneno mawili. Tuko pamoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Waziri?

Ibara ilikuwa imeshahojiwa hii. Sawa tumemaliza.

Waheshimiwa Wabunge, tuko kifungu cha nane. Ulikuwa umeshakisoma Katibu? Haya twende cha 8.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 31

**MWENYEKITI:** Haya, Waheshimiwa Wabunge Kifungu cha 31 kina marekebisho ya Serikali kwenye yale maneno ya pembeni, pia kwenye sehemu ya Kifungu kidogo cha kwanza, yanafutwa maneno "itakuwa na jukumu la", na maneno haya yakishafutwa yanakuwa na neno "inaweza." Kwa hiyo, yatasomeka, "mamlaka inaweza kushauri kuhusu uendeshaji wa viwanja binafsi vya ndege vya Tanzania Bara." Wakati mwanzo ilikuwa, "itakuwa na jukumu." Kwa hiyo, wanaweka, maneno "inaweza" badala ya maneno ya "itakuwa na jukumu la."

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 38

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Marekebisho ya Serikali yanafuta kifungu kidogo cha (a)(i) ambacho kilikuwa kinasema, "Anapatikana katika eneo lolote la kiwanja cha ndege." Hilo linaondolewa. Kwa hiyo, hapo tutafanya namba upya. Kwa hiyo, kutakuwa na 1 na 2; na kifungu cha 3 kitakuwa hakipo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kwagilwa ana marekebisho katika Sura ya Sita, anaongeza Sura ya Sita mpya.

**MWENYEKITI:** Marekebisho ya Mheshimiwa Kwagilwa ameniletea ujumbe kwamba ameyaondoa. Kwa hiyo, ameyaondoa marekebisho yake yote. *(Makofi)*

Tunaendelea.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Jedwali la 1
Jedwali la 2

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bado lile jina refu. *AG* tumeshaipata? Haya, hebu tuletee hapa tuone inasomeka namna gani? Pia, Mheshimiwa Dkt. Kimei hebu tuangalizie kwenye ile sheria tuliyotunga ya mamlaka uliyosema, inaweza ikatupatia mwongozo hapa pia. Haya, ahsante.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza isomeke "Sheria ya Kuweka Masharti kwa ajili ya Uanzishaji, Uendelezaji, Usimamizi, Uendelezaji na Utunzaji wa Viwanja vya Ndege, Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu na Mamlaka yake na Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo."

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, mmerejea kwenye neno masharti, si ndiyo!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, tumeondoa madhubuti.

**MWENYEKITI:** Ahaa, haya. Hebu naomba hicho ulichokisoma hapo.

Haya, Waheshimiwa Wabunge, hapa maneno yanabaki katika jina refu, "Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji, Uendelezaji, Usimamizi, Uendeshaji na Utunzaji wa Viwanja vya Ndege..." na maneno mengine yanayoendelea hapo, kama "kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na kuainisha majukumu na mamlaka yake na masuala mengine yahusianayo na hayo."

"Kuainisha majukumu," sasa hapa neno 'mamlaka' limerudi tena. Hii kwenye mamlaka yake au hapa tuliache! Ama na hapa iwe na madaraka yake? Kiswahili kigumu kweli.

Hapa linabaki? "Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na kuainisha majukumu na madaraka yake" kwa maana ya *powers,* si ndiyo? Hamna neno, itakapokuja hiyo nyingine itatusaidia kwenye tafsiri. Tupo katika kujifunza kutunga sheria kwa Kiswahili. Kwa hiyo, mambo mengi tutajikuta tunaenda nayo.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tukubaliane na hili pendekezo. Kama kutakuwa na sababu ya kubadilisha kwa sababu ni neno, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuna sheria ambayo imetungwa na Bunge inayompa fursa kufanya marekebisho madogo kama hayo. Kwa sasa hapa paitwe jina refu, "Sheria ya Kuweka Masharti kwa ajili ya Uanzishaji...", hivi haya maneno 'kwa ajili' nani kaongeza tena? *(Kicheko)*

"Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji," hii 'kwa ajili' Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutoe?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sawa.

**MWENYEKITI:** Haya. Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji, Uendelezaji, Usimamizi, Uendeshaji na Utunzaji wa Viwanja vya

Ndege, Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu na Madaraka yake na Masuala Mengine yanayohusiana na hayo." Sawa? *(Makofi)*

Haya. Ahsante sana.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nione ile Sheria ya Manunuzi. Ile Sheria ya Manununzi kwa isivyo bahati kwenye Kamati yetu ya Bajeti tulikuwa tume-*suggest* kwamba, iwe ni "madaraka ya mamlaka", lakini naona ilikuja kubakia "mamlaka ya mamlaka." *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebakia mamlaka ya mamlaka lakini tulikuwa tumependekeza…

**MWENYEKITI:** Sawa. Kama nilivyosema, tupo kwenye mchakato wa kutengeneza sheria kwa Kiswahili, jambo ambalo litaendelea kuwa kwenye mafunzo kwa muda kidogo. Kwa hiyo, sasa tumejifunza kwamba hayo mawili ukiyaunganisha yanaleta hiyo changamoto.

Mwanasheria mwingine amesimama.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulitunga Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Kiswahili.

**MWENYEKITI:** Nini?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lilitunga Sheria ya Tume ya Mipango na tulitunga kwa Kiswahili. Sasa labda tuki-*borrow* hiyo *construction* yake, badala ya kuorodhesha haya mengi sana kwa sababu inaendelea, tungesema tu ni "Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Kuainisha Majukumu Yake na Mamlaka Yake na Kuainisha Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo." Halafu hayo sasa ya usimamizi na nini vitakuwepo kwenye vifungu vinavyohusika, ikawa *short*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuna muda hata mimi nilifikiri hivyo, lakini niliiona changamoto baada ya kugundua kwamba huu uanzishaji siyo yenyewe ndiyo inayofanya. Yenyewe itafanya kazi ya kusimamia kwa sababu kuna watu wanaaanzisha viwanja vya ndege binafsi. Kwa hiyo, nikaona kama tukiifupisha, inaweza kuja na hiyo picha.

Hebu tuitazame sote kwa pamoja kwa sababu tofauti na hii Tume, hii Tume ina shughuli yake moja tu na imenyooka, yaani kwa maana ya kwamba, wote tunajua lakini hawa wanaweza kuwa na hayo.

Sasa si…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hii yote kuna kuanzishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, ipo ndani…

**MWENYEKITI:** Ndiyo, ipo hapa.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** …ambayo ndiyo kubwa kwa maoni yangu.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mengine "ili kuweka masharti ya uendelezaji, usimamizi" ingeweza ku-*fall* kwenye masuala mengine yanayohusiana na uanzishwaji wa hii Mamlaka. Kwa hiyo, kama tuki-*borrow* hiyo *construction* ya hii Sheria ya Mipango, tukisema, kama kweli Mamlaka ndiyo kubwa, (uanzishwaji wa mamlaka), tukasema, "Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, kuainisha majukumu yake na mamlaka yake...," halafu tukaendelea sasa na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo ya "usimamizi, uendelezaji, Madhubuti" na vitu kama hivyo, nadhani wataendeleza kwenye vifungu vya sheria na iwe *short* bila

kufanya ikaonekana kwamba huu uanzishwaji na usimamizi ndiyo mkubwa kuliko *actually* hii *agency* ambayo inaanzishwa.

**MWENYEKITI:** Sasa hapa tusaidiane. Kwanza, huu uanzishaji ni hii Mamlaka inaanzisha au Mamlaka itakuwa ina vyake inanzisha na wengine wanaanzisha? Tuelewane hapo.

Mheshimiwa Waziri, ili tujue kama haya maneno ya mwanzo tuyafute, ni hii mamlaka ndiyo itakuwa inasimamia uanzishaji na viwanja vyote vya ndege au kuna ambavyo vinaweza kuanzishwa bila Mamlaka?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes,* ni sahihi. Kuna baadhi ya viwanja vitaanzishwa na *private sector,* lakini *specific* hapa tunazungumzia Viwanja vya Serikali. Serikali leo inaweza kuamua kuanzisha kiwanja mji fulani, na hiyo ndiyo kazi ya Mamlaka hii lakini *private sector* wanaweza kufanya jambo lao na vipo viwanja vingi sasa hivi vinasimamiwa na *private sector*. Wanaweza kuendeleza ama kuanzisha kwa kupata kibali kutoka *TCAA*.

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mbunge ni kwamba, hii sheria tukiichukua tukiacha hii *long form* tukaichukua hii sheria, inahusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na kazi zake na nini ndicho kilichomo humo ama humu kimo na ambacho kipo nje ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege? Ili tukipatie uzito kile ambacho sheria hii imekuja kufanya, halafu mengine yale tuyafanye ni ya ziada. Ndiyo hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ni utekelezaji wa Mkataba wa Chicago wa Mwaka 1944 kiambatisho cha 14, ambayo inataka nchi wanachama na *signatory* wa *Chicago Convention* wawe na sheria inayoweka masharti ya uanzishaji, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege. Pia, mkataba ule unataka kwamba nchi mwanachama iwe na taasisi mahsusi ambayo itakuwa inasimamia kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia *actually* ni *caption* ya *Annex 14* ya *Chicago convention*. Kwa hiyo, nilivyokuwa nafikiri, hivi ilivyokaa ni sawa. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa je, kwa mfano, tungeanza na "Sheria ya Uanzishaji wa Mamlaka ama Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu na Madaraka yake (kama alivyosema) na masuala mengine yahusianayo na hayo," tunakuwa tumeenda kinyume na ule mkataba au haya ya uanzishaji wa hivyo vya binafsi pia yatakuwemo, uendelezaji wa vya Serikali na vya binafsi umo, usimamizi umo, uendeshaji umo, utunzaji wa viwanja vya ndege pia umo?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kidogo.

**MWENYEKITI:** Unatokea wapi? Haya, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na tulijadili hilo suala ambalo lipo Mezani sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka, tunazo aina mbili za utungaji wa sheria. Kuna utungaji wa sheria wa kuanzisha mamlaka, ni kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge watakumbuka, mwaka 2023 tulipitisha Sheria ya Uchaguzi ambayo inaweka Masharti ya Uchaguzi na Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Zilikuwa ni sheria mbili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, alichoongea Mheshimiwa Mbunge aliyetoa hoja, ilikuwa ni mfumo ule wa sheria ya kuanzisha taasisi, lakini hii sheria ni Sheria ya Viwanja vya Ndege, siyo Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kwa hiyo, hata sisi kwenye Kamati yetu tuliridhika na hii *submission* kama ilivyo, kwamba sheria hii ni ya kutengeneza masharti pamoja na kuanzisha mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunapendekeza ibaki hivi ilivyo kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naona makofi. Tatizo hapa asubuhi kuna makofi yamepigwa, nusura niulize sasa haya makofi yanaashiria nini? Mheshimiwa Geoffrey Mwambe tusaidie. Tukianzia hapa kwenye kuanzisha hii mamlaka, "Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, kuainisha majukumu na mamlaka yake na masuala mengine yanayohusiana na hayo." Humo ndani yanakuwa hayamo haya mengine haya ya usimamizi, uendeshaji na kadhalika?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, eneo la kwanza la sheria hii ni kutambua utaratibu wa uendeshaji wa viwanja vya ndege hasa vya Serikali kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alizungumza, ndiyo eneo la msingi, ndiyo eneo kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *of course*, ukiangalia *layout* ya sheria ungeweza kusema ingetakiwa ianze *part two* baada ya tafsiri, ilitakiwa ianze "masharti ya uendeshaji wa viwanja vya ndege," halafu baadaye ndiyo *part three* iwe "uanzishaji wa mamlaka ya kusimamia hayo masharti hapo juu." Ingawa *of course* tukasema kwenye utungaji sasa inaweza ikawa vyovyote vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo kubwa ni kuanza na masharti, viwanja vya ndege viweje, usimamizi wake utaratibu na nini halafu ndiyo iwe nani atakayesimamia viwanja vya ndege.

**MWENYEKITI:** Sawa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *in any case,* hii ni *long title*. Huwa inaitwa *long title for a reason*. Kwamba inaweza humo mambo yote unayotaka yawemo, unaruhusiwa kuweka kwa sababu ni *long title;* lakini hapa pengine Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kama haitaleta shida ili tusianze sasa kuipangua sheria, hii sheria ianze na hilo ambalo linaonekana ni kubwa zaidi ambalo ni kuanzisha mamlaka, halafu haya ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya

ndege, hapa kuna vya Serikali, vitaingia na hivyo vya binafsi; ninaona huku mbele kuna viwanja. Ina shida yoyote kukifanyiwa *re-arrangement* ya hii *long tittle*?

Kwamba, kwanza ina-*establish* mamlaka, halafu inafanya na haya mengine ila yawepo kwenye *long title*. Kwa maana ipi? Tuanze na Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu na Madaraka yake na tunarudi, kuweka masharti ile ambayo sasa umeleta, masharti yale yote yaambatane. Si ndiyo eh, ili tusiyapunguze hayo maneno. Inaitwa *long title for a reason*.

Waheshimiwa Wabunge, ngoja aandike vizuri Katibu maana itabidi asome hii *long tittle* inafananaje halafu tutakamilisha hii kazi. Haya, Katibu tusomee namna itakavyosomeka.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu, Madaraka na Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendelezaji, Usimamizi na Uendeshaji Utunzaji wa Viwanja vya Ndege na Masuala mengine yanayohusiana na Hayo."

**MWENYEKITI:** Umesahau neno 'yake' hebu tusomee.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kuainisha Majukumu na Madaraka Yake na Kuweka Masharti ya Uanzishaji, Uendelezaji, Usimamizi, Uendeshaji na Utunzaji wa Viwanja vya Ndege na Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo."

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hilo ndiyo jina refu kwa kadri lilivyorekebishwa. Si tunakubaliana?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Yuko wapi?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwambe bado.

**MWENYEKITI:** Ehe, naam.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutachukua hiyo *long title* ya namna hiyo, basi itatulazimisha turudi kwenye *short title* kuwa ni Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na siyo Sheria ya Viwanja vya Ndege kama ilivyo sasa. Kwa sababu sasa *emphasis* imekuwa ni uanzisaji wa mamlaka.

**MWENYEKITI:** Inakuwa iko sawa, kwa sababu namna tulivyoipanga sheria, tumeanza na uanzishaji wa mamlaka.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, kwa hiyo...

**MWENYEKITI:** Si ndiyo sheria yetu ilivyopangwa, ama mimi niko nayo tofauti hapa? Hebu nenda kwenye sheria yako wewe, nakala yako inasemaje ya sheria yote?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *in fact* mimi ndiyo nilichokisema hicho hicho. Nilisema kwamba kwa sheria...

**MWENYEKITI:** Basi hicho hicho ndiyo kinachotufanya tuanzie na hapa kwa sababu, la sivyo inabidi tukaipindue sheria. Sasa kuliko tupindue sheria, bora tupindue *long title*.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *short title* ibaki vilevile?

**MWENYEKITI:** *Short title* inabaki hivyo hivyo.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Viwanja vya Ndege!

**MWENYEKITI:** Naam.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** *Okay*.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria Ibara kwa Ibara na imekubali kama ilivyopitishwa na marekebisho yake na Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024, sasa ukubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nitawahoji, wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kuhusu Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa mwaka 2024.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Viwanja vya Ndege Tanzania na kuainisha majukumu na madaraka yake na kuweka masharti ya uanzishaji, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, Sheria yetu hii ama Muswada wetu huu umepitishwa rasmi na Bunge baada ya kuwahoji na Wabunge wengi kusema ndiyo, kwa hiyo, natumia nafasi hii kusema Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024 umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Hivyo, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na Watendaji wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri sana ambayo mmeifanya ya kuleta Muswada huu ambao Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanashauri kwenye hayo Mabunge yaliyopita. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi hii nzuri mliyoifanya ya kuhakikisha Muswada huu unafika mbele ya Bunge na umeweza kupitishwa.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo tunawashukuru kwa ushirikiano ambao mmeutoa kwa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, mawazo waliyoyatoa mmeyaweka humo na wao wameridhika kabisa, kwa hiyo tunawashukuru.

Wakati huo huo kuna mambo mawili ambayo Wajumbe wa Kamati kwenye taarifa yao wameonesha kwamba yanahitaji

bado kuendelea kufanyiwa kazi. Moja ni hili eneo la Zimamoto. Pamoja na kwamba sheria leo imeshatungwa, lakini na sisi kwa sababu kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali hatujitazami peke yetu, tunatazama na wenzetu, basi tujaribu kuangalia uzoefu wa hayo maeneo mengine wanafanyaje kwenye hili eneo la Zimamoto?

Pengine siyo lazima kuanzisha kitu kingine kabisa kwamba ni Jeshi, hata kama wanatoka huko Jeshi letu la Zimamoto lakini wanapokuja huku, basi wawe ni watumishi ambao wanaweza kuchukuliwa hatua zile ambazo ni za kawaida, ukiacha za Kijeshi ambazo itabidi mwarejeshe kwenye Jeshi, lakini kwa maana ya kwamba mahali ambako wanakuwa wanajua ndio mwajiri wao, wajue mamlaka ndiyo mwajiri wao ili wasiwe wanajikuta kwamba wako kwenye majukumu mengine kama ambavyo tumepewa mifano hapa, kwamba anakuwa anatafutwa eneo lake la kazi lakini anaambiwa kwamba ametumwa na Afande mwingine sehemu nyingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mazingira kama hayo yataleta changamoto na mtazame huko kwingine wanafanyaje? Kama ni lazima kuwepo kwenye sheria, basi mtalileta ili tulifanyie kazi, lakini kama siyo lazima, basi katika ule utendaji mwangalie namna gani mtawasiliana na Jeshi la Zimamoto ili liwapatie hawa wafanyakazi wawe chini yenu na ninyi muweze kuwa mnawafuatilia kwenye kazi zao. *(Makofi)*

Jambo la pili lililozungumzwa ni kuhusu mapato kwenye hilo eneo moja ambalo wale abiria wanaotumia hii huduma ya usafiri wa ndege wanalipa, kwamba ibaki kwa mamlaka ili huduma nyingine zile ambazo ni za haraka ziweze kutolewa kwa wakati.

Sasa, hili nalo mlitazame kwa sababu tangu kipindi ambacho haya mabadiliko, uzuri ni kwamba yote yameshawahi kuwepo. Yameshawahi kuwepo mazingira ambayo fedha hizi zilikuwa zinakusanywa na mamlaka na yameshawahi kuwepo mazingira ambayo fedha hizi zilikuwa hazikusanywi na mamlaka, halafu sasa baadaye tena mawazo yamekuja mapya. Kwa hiyo,

siyo jambo jipya kwenda mbele na kutazama hatua zako kama unaenda sawasawa ama sivyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninyi mfanye sasa tathmini kama kipindi kipi inaonekana viwanja vya ndege vilikuwa bora zaidi, kwa nini? Kwa sababu huko tunakoelekea tunataka viendelee kuwa bora zaidi. Ndege zetu zinaendelea kuleta abiria wanaotoka maeneo ya mbali zaidi na ndege zinaongezeka. Kwa hiyo, viwanja vyetu pia lazima viwe bora na ubora ule lazima ufanane na huko kwingine ambako ndege zetu zinaenda kutua. Kwa hiyo, mtazame hayo mazingira yote mwone kipindi gani ambacho viwanja vyetu vilikuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri ametoa hapa ufafanuzi kwamba Serikali inatoa fedha nyingi kuliko hata hizo ambazo zingepatikana kwenye hili eneo la fedha inayotolewa na abiria anayetumia viwanja vya ndege. Ni kweli, lakini sasa tunajaribu kuona mazingira ambayo fedha zinazokwenda ni nyingi lakini zinahusu ujenzi wa viwanja hivi, ujenzi wa majengo haya. *(Makofi)*

Sasa kuna Mbunge amesema, hili jengo linapoanza kuvuja, hatuna hakika kama yale mabilioni yaliyotajwa yanaenda kwa haraka kwenye mamlaka kuweza kufanya hayo marekebisho. Sasa, kwa sababu hatuna hakika, ndiyo maana Kamati imependekeza mwendelee kulifanyia kazi jambo hili, na nafikiri ni la muhimu kwa sababu eneo la kusafirisha abiria ni eneo la ukarimu. Kwa hiyo, watu kuna mambo madogo madogo sana ambayo huwa yanaleta changamoto. *(Makofi)*

Kama hili ni eneo linaloleta changamoto, basi mlifanyie kazi mwone namna ambavyo tunaweza kufanya marekebisho, lakini kama halina changamoto, basi ni vema na tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge, utekelezaji utaanza kama ilivyo ada Mheshimiwa Rais atakapokuwa ametoa kibali kwa sheria hii kwa kuisaini kama ambavyo Katiba yetu inataka.

Baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya mpaka tumefika hapa leo, ahsanteni sana.

Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushiriki wenu katika kuchangia hapa ndani na wengine mlitoa mawazo yenu huko nyuma na yamesaidia Muswada huu kukamilika na hata leo kupitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge tunao wageni walioko Bungeni ambao hawakupata nafasi ya kutangazwa wakati tukitangaza tangazo la mwanzo.

Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika na tutaanza na Mheshimiwa Marianne Young ambaye ni Balozi wa Uingereza Nchini Tanzania, karibu sana, ahsante sana. Ameongozana na Ndugu Godfrida Magubo ambaye ni Mkuu wa Ofisi Ndogo ya Ubalozi Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Isha Shelat ambaye ni Mkuu wa Mawasiliano Ubalozi wa Uingereza, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Noel Mtafya, Afisa Mambo ya Nje, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Glory Mndolwa, Afisa Mambo ya Nje, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ahsante sana. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 106 na walimu 10 wa Shule ya Awali na Msingi ya Mwalimu Anna kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tumehitimisha shughuli zile ambazo zilikuwa zimepangwa kwenye

ratiba ya leo, kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 29 Agosti, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*